## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA YA NGUJINI KWA ROBO YA KWANZA JULY-SEPTEMBER 2017/2018 KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE 14/11/2017.

### UTANGULIZI

Kata ya Ngujini ni mojawapo ya kata kati ya kata ishirini zilizopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

**MIPAKA:** Kata ya Ngujini inapakana na kata za Shighatini (Kaskazini), Chomvu (Mashariki), Lembeni (Kusini-Magharibi) na Kilomeni (Kusini Kashariki).

**UTAWALA:** Kiutawala kata ya Ngujini ina vijiji vitatu; Ngujini, Songoa Na Chanjale.

**ELIMU:** Kata ina jumla ya shule nne (4) za msingi: Kisangara juu, Kitivoni, Songoa na Changalavo. Shule mbili (2) za sekondari: Ngujini (Serikali) na Kindoroko (Binafsi)

**AFYA:** Zahanati tatu: Ngujini na Songoa (Serikali) na Kisangara Juu Parish (Binafsi).

### ULINZI NA USALAMA

Hali ni shwari.

Uhusiano wa wakulima na wafugaji ni mzuri.

Hifadhi ya mazingira ni nzuri.

### VIKAO VYA KISHERIA NA MIKUTANO NGAZI YA KATA, VIJIJI NA VITONGOJI

**(i) VIKAO VYA WDC.**

| NA. | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ngujini | 1 | 1 | |

**(ii) VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA KIJIJI**

| NA. | KATA | KIJIJI | VIKAO | | MIKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| 1 | Ngujini | Ngujini | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| 2 | | Chanjale | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| 3 | | Songoa | 3 | 3 | 1 | 1 | |

**(iii) MIKUTANO YA WAKAZI VITONGOJI**

| NA. | KATA | KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ngujini | Ngujini | 5 | 15 | 15 | |
| 2 | | Chanjale | 3 | 9 | 6 | |
| 3 | | Songoa | 2 | 6 | 4 | |

## MAPATO NA MATUMIZI

### (i) TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI ZILIZOSOMWA KWENYE MIKUTANO MIKUU YA VIJIJI

Kipindi cha robo ya NNE 2017/2018 taarifa za mapato na matumizi zilizosomwa na kukubalika kwenye mikutano mikuu ya vijiji ni kama ifuatavyo;-

| NA. | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ngujini | 7,500000.00 | 5,824,500.00 | 73% | Ujenzi nyumba ya mwalimu |
| 2 | Chanjale | 2,416,000.00<br>200,000.00 | 2,416,000.00<br>175,000.00 | 100%<br>87.5% | TASAF<br>TASAF imetoa kwa H/kijiji |
| 3 | Songoa | 884,000.00<br>30,000.00 | 884,000.00<br>30,000.00 | 100% | TASAF<br>TASAF imetoa kwa H/kijiji |

### (ii) MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA

Kipindi cha robo ya NNE 2017/2018 vijiji vya Kata ya Ngujini vilikusanya mapato ya halmashauri ya wilaya kama ifuatavyo;-

| NA. | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ngujini | - | 24,000.00<br>48,600.00 | -<br>- | Mapato ya Lesseni<br>Ukaguzi wa Nyama |
| 2 | Chanjale | - | - | - | |
| 3 | Songoa | - | | | |
| | **JUMLA** | | **72,000.00** | | |

### (iii) MAPATO YA HALMASHAURI YA KIJIJI

**Tshs. 30,000/=** za kodi ya pango zilikusanywa na kijiji cha Ngujini.

## MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA

### (i) MIRADI YA MAENDELEO

Ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya Msingi Changalavo umefikia hatua ya Msingi na Jamvi na vifaa vya kupandisha kuta mpaka renta vyote vipo site.

Michango ya wananchi ujenzi wa maabara Ngujini Sekondari- kijiji cha Songoa Tshs 76,000/=, Ngujini Tshs 136,000/= na Chanjale Tshs 230,000/= **JUMLA Tshs 442,000/=**

Aidha uendelezwaji wa ujenzi wa maabara utaanza mara moja mwezi wa kumi baada ya maafali ambayo yataambatana na harambee ya kuchangia ujenzi wa maabara.

### (ii) TAARIFA ZA KISEKTA

**ELIMU MSINGI NA SEKONDARI**

Kufanyika kwa mtihani wa darasa la Saba

Ufundishaji madarasani kwa mujibu wa sheria.

Upokeaji wa ruzuku toka serikalini ambapo **Jumla ya Tshs 3,415,661.86** zilipokelewa kwa Shule za Msingi na **Tshs 1,072,543.05** zilipokelewa Sekondari ya Ngujini
Huduma ya chakula cha mchana kwa Shule za Sekondari 2 na Msingi 3.
Kufanyika kwa vikao vya wazazi, Bodi ya wazazi na kamati za shule.
Kuanza ujenzi wa nyumba ya mwalimu Shule ya msingi Changalavo.
- Choo cha shule ya Kitivoni, Kilatogali yanachomwa na kijengo

**SEKTA YA AFYA**

Huduma ya Matibabu kwa wagonjwa **163** Zahanati ya Songoa na **390** Zahanati ya Ngujini
Utoaji Elimu ya afya na upimaji wa Virusi vya Ukimwi (VVU).
Huduma ya Chanjo kwa watoto chini ya miaka mitano.
Ufuatiliaji maendeleo ya ukuaji wa watoto chini ya miaka mitano.
Huduma ya kliniki ya wajawazito na watoto
Uchangiaji wa i**CHF Zahanati ya Songoa-60,000/=** na **Zahanati ya Ngujini-210,000.00**

**SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO**

Wakulima 732 na wafugaji 747 walipata ushauri wa kitaalamu.
Ukaguzi wa nyama kabla kufika kwa walaji (Ng'ombe 26, Kondoo 12).
Matibabu kwa Ng'ombe 31, Mbuzi 43 na Kuku 207 ambapo Vifo ni Mbuzi 7 na Kuku 15.

**MAFANIKIO, CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO KWA UJUMLA**

**(i) MAFANIKIO KWA UJUMLA**

Baadhi ya wakulima kukubali kufufua zao la kahawa katika msimu wa mvua za mvuli.
Wananchi kushiriki katika shughuli za kimaendeleo.
Uwepo wa dawa muhimu katika zahanati zote mbili.
Shule za Sekondari na msingi 3 kutoa huduma ya chakula cha mchana.
Wakulima na wafugaji wamepewa ushauri wa kanuni bora za kilimo na ufugaji.
Kuendelkea kuwepo kwa usalama wa kuridhisha.
Kupungua kwa uharibifu wa ndani ya hifadhi ya msitu wa kindoroko.

**(ii)CHANGAMOTO KWA UJUMLA**

Mwitikio mdogo wa wananchi kujiunga na iCHF.
Ubovu wa miundombinu ya barabara.
Ukosefu wa rasilimali fedha kukamilisha ujenzi wa Maabara mbili (2) Ngujini Sekondari.
na ukamilishaji wa zahanati ya Changale na Hostel Ngujini S

**(iii)MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko iCHF
Kwa ushirikiano wa Halmashauri ya wilaya na wananchi kuondoa tatizo la ubovu wa miundombinu barabara
Wananchi na Halmashauri wilaya kushirikiana kuondoa tatizo la ukosefu wa Maabara Sekondari

**HITIMISHO**

Kata ya Ngujini tunaomba sana barabara zetu zinazounganisha kata za Lembeni Ngujini na Shighatini walau zikwanguliwe kwa greda ili ziweze kupitika vizuri hasa barabara ya Chanjale Chini, Chanjal juu Mpaka Ngujini hali ni mbaya sana.

Naomba kuwasilisha.

THERESIA P. MSUYA
DIWANI/MWENYEKITI-WDC

IMANI Y. MWANDUMBYA
WEO/KATIBU-WDC

AFISA MTENDAJI
KATA YA NGUJINI

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA,TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO KATIKA KATA YA MSANGENI KWA KIPINDI CHA ~~AGOSTI HADI OKTOBA 2017~~** 14/11/2017

Jully ~~Ag~~ – September 2017

**UTANGULIZI**

Kata ya Msangeni iko katika Tarafa ya Ugweno Wilaya ya Mwanga.

I. **MIPAKA:**

Upande wa kusini na mashariki inapatikana na kata ya jipe. Magharibi inapakana na kata ya shighatini. Kwa upande wa kaskazini inapakana kata ya kifula.

II. **UTAWALA:**

Kata ya Msangeni ina vijiji 5 ambavyo ni Simbomu, Mruma, Mwai, Mamba na Msangeni.

III. **ELIMU:**

Kata ya MSANGENI ina shule za msingi 7 ambazo ni Simbomu, Mruma, Mwai, Mamba Msangeni,Sungo, na KaseniShule za sekondari ziko tatu(3) ambazo ni Simbomu,Msangeni na Mruma inayomilikiwa na Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)

IV. **AFYA :**

Kata ya Msangeni ina Zahanati (4) nne ambazo ni Mwai,Kyanga, Kikweni na Sungo.

V. **UCHUMI :**

Njia kuu za uchumi katika kata ya Msangeni ni Kilimo, Ufugaji mdogomdogo, biashara ndogo ndogo na ajira rasmi. Kata ina wakazi zaidi ya elfu sita (6000).

1 – **ULINZI NA USALAMA KATIKA KATA YA MSANGENI**

Kwa upande wa binadamu hali ni shwari ila kwa upande wa mali, kuna wizi ulioripotiwa katika shule ya sekondari Msangeni ambapo watu walisadikika ni wezi walivunja ofisi ya mkuu wa shule na kuiba kompyuta tatu na kuvunja dirisha na makufuli ya kabati . Taarifa ilifikishwa katika kituo cha polisi na walinzi wawili walihojiwa nakuachwa huru na uchunguzi bado unaendelea . Pia wizi wa kuku umeripotiwa katika vijiji vya Mruma, Simbomu na Mamba.

Kikao cha WDC kiliwataka viongozi wa vijiji vyote kukomesha mara moja wizi huo kijiji cha Mruma kimepiga marufuku pikipiki kuingia na kutoka kijijini hapo baada ya saa 4:00 (nne kamili) usiku.

**VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA, KIJIJI NA VITONGOJI**

Majwedwali chini yanaonyesha vikao hivyo kwa ngazi husika.

I) **VIKAO VYA WDC**

| NO | LENGO | HALISI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | |

## VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI

### A. MIKUTANO MIKUU

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAI | 1 | 1 | |
| 2 | SIMBOMU | 1 | 1 | |
| 3 | MRUMA | 1 | 1 | |
| 4 | MAMBA | 1 | 1 | |
| 5 | MSANGENI | 1 | 1 | |

### B. MIKUTANO YA MAPATO NA MATUMIZI

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAI | 1 | 1 | |
| 2 | MRUMA | 1 | 1 | |
| 3 | SIMBOMU | 1 | 1 | |
| 4 | MAMBA | 1 | 1 | |
| 5 | MSANGENI | 1 | 1 | |

### C. MAPATO HALISI YA WILAYA

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAI | | | | |
| 2 | SIMBOMU | | | | |
| 3 | MRUMA | | | | |
| 4 | MAMBA | | | | |
| 5 | MSANGENI | | | | |

### MAPATO YA VIJIJI

| NO | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAI | | | | |
| 2 | SIMBOMU | | | | |
| 3 | MRUMA | | | | |
| 4 | MAMBA | | | | |
| 5 | MSANGENI | | | | |

### MIKUTANO YA MAKAZI WA VITONGOJI

| SN | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| **1** | MWAI | 9 | 6 | |
| **2** | SIMBOMU | 6 | 4 | |
| **3** | MRUMA | 12 | 9 | |
| **4** | MAMBA | 12 | 10 | |
| **5** | MSANGENI | 18 | 14 | |

**MFUKO WA AFYA YA JAMII ILIYOBORESHWA ( iCHF)**

| SN | IDADI YA WACHANGIAJI(KAYA) | | JUMLA YA FEDHA TSHS | MAWELEZO |
|---|---|---|---|---|
| | KIJIJI | KAYA | | |
| 1 | MWAI | 6 | 180,OOO | |
| 2 | KYANGA | 7 | 210,000 | |
| 3 | KIKWENI | 10 | 300,000 | |
| 4 | SUNGO | 9 | 270,000 | |

960,000/=

- Wachangiaji wengi wamechangua kituo cha afya cha Kifula kama kituo cha msingi na kukosesha mapato katika zahanati za kata ya Msangeni

**MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA:**

Kata ya msangeni ina miradi mingi ya maendeleo kama ifuatavyo:

a. **BARABARA**

Kijiji cha Mruma ~~wanakijiji~~ wanachimba barabara itokayo Mfwere hadi Msangeni yenye urefu wa km 2.5 na wameshachimba km1.4.

Kijiji cha mamba wanachimba barabara mbili;

i) Marundu –,Msangeni km 2 wameshakamilisha uchimbaji na taratibu za kumwona Mhandisi kwa marekebisho zinaendelea

ii) Barabara ya Lungwa - Ngorio imeshakamilika ila kuna korongo la sawe linaloendelea kushindiliwa kwa nguvu za wanakijiji. wanashida ya Makalvert mawili

Kijiji cha Msangeni kinachimba barabara ya Tongo –Misumbwini kuungana na barabara ya Chunguli –Butu. Wameshachimba km-2 ¾ na inaendelea kupanuliwa.

Pia kuna mradi ya ujenzi ~~kama vile~~ wa

a) Ofisi ya walimu shule ya msingi Msangeni,

Mradi huo ulishulikiwa na wananchi kupitia harambee iliyoongozwa na Afisa Elimu msingi (W), Mh. Diwani viongozi wa kata na kijiji cha Msangeni. ~~Hongereni~~ wahusika.

Kamati ya maendeleo ya kata ya Msangeni (WDC) inawaomba walioahidi kuchangia ofisi hiyo wafanye hivyo ili kupunguza madeni yanayotokana na ahadi hizo. Wamechangia sh…2,474,100/=……wakatumia sh…2982,100/=……nawanadaiwa sh……508,000/=…… DENI

(b) – Nyumba ya Walimu shule ya msingi Sungo imeshawekwa umeme kupitia harambee iliyoongwazwa na Mh. Diwani ili mwalimu aishi shuleni, tunaomba saruji na ceillingbord kwa ajili ya umaliziaji wa nyumba hiyo. ~~Zahanati ya Kikweni ni~~

Harambee mapato 1133000/=
Matumizi 1207000/=
DENI 74000/=

ZAHANATI YA KIKWENI

kongwe, ceillingbord zake zimeanza kuanguka.Tunaomba msaada wa vifaa vya viwandani ili ikarabatiwe .Zahanati ya mwai haina nyumba ya wauguzi. Wameshaanza kujenga msingi. Tunaomba vifaa vya viwandani ili hiyo nyumba ikamilishwe

## MIRADI YA MAJI

Kijiji cha Mamba kimeshachimba mtaro na kufukia mabomba toka Msangeni hadi Sungulini kwenye tanki watapata maji safi wakati wowote kuanzia sasa.Utafiti wa maji umefanywa kijijini Mruma na uchimbaji utaanza tathimini itakapofanyika.

## HUDUMA ZA KIFEDHA

Kata ina **SACCOS** moja iliyoko Msangeni inayotoa huduma kata nzima.

## KILIMO

- Katika kipindi hicho ushauri wa kilimo uliendelea kutolewa na wakulima wengi wamepokea ushauri huo na kufanyia kazi kama vile kuandaa mashamba mapema, kupanda kwa wakati na kutumia mbegu bora na za muda mfupi kulingana na hali ya hewa
- Vilivile vikundi vya wakulima vilipatiwa mafunzo mbalimbali (kikundi cha simbomu &kikundi cha msangeni) mada zilizo fundishwa ni pamoja na kilimo cha mahindi bora, hifadhi ya udongo, ufugaji bora wa kuku wa kienyeji na matumizi bora ya mbolea na viuatilifu Aidha juhudi za kuunda vikundi vingine bado zinaendelea katika vijiji vingine.
- Uhamasishaji wa zao la kahawa unaendelea na wakulima wamehamasika na kuchanga pesa zao kwa ajili ya kununua miche ya kahawa .Fedha zilzokusanya niTsh.57,000/= ,kwa ajili ya miche ipatayo 380. Aidha wakulima wengine wamepatiwa miche ya kahawa kupitia chama cha ushirika cha **VUASU.**

## MIFUGO

i) Matibabu ya wanyama yamefanyika kwa kutibu magonjwa mbalimbali;

a) Maganjwa yaletwayo/yanayosababishwa na bacteria kama Mastitis
b) Magonjwa yanasababishwa na protozoa kama Anaplasmosis na Trypanasomiasis.
c) Magwanjwa yanayosababishwa na parasites wa nje na ndani ya mwili kama Minyoo na Mange & Mites

ii) Chanjo zilizofanyika;

a. Chanjo ya kideri na mdondoo kwa kuku
b. Chanjo ya homa ya mapafu kwa mbuzi na kondoo

iii) Ushauri wa lishe na matibabu kwa muda unaokubalika, pia kuhamilisha ili kupata mifugo bora yenye tija katika uzalishaji wa nyama na maziwa

iv) Ukaguzi wa nyama umefanyika na walikaguliwa jumla ya ngombe 26 sawa na kiasi cha sh 39,000/=

**AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA**

Shughuli zilizofanyika ni ukaguzi wa vyoo bora na vya asili kwenye kaya, matumizi ya vibuyu chirizi na usafi wa jumamosi ya mwisho wa mwezi umefanyika. Ugukazi wa pombe kali (viroba) umefanyika kwa kila duka na baa na hazikupatikana.

Kwa kushirikiana na maafisa watendaji wa vijiji ukaguzi wa maduka ulifanyika kulingana na sheria ya TFDA mwaka 2003. Pia ukaguzi wa majengo ya biashara zote ulifanyika na kuwasajili wafanya biashara kupatiwa vibali vya TFDA. Jumla ya fedha zilizokusanywa kwa ajili ya vibali vya TFDA ni sh 550,000/=

**UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

Wakazi wengi wa kata ya Msangeni wanaendelea kupanda miti katika msimu huu wa mvua za vuli. Miti aina ya Acrocarpus ipo katika vyanzo vya maji na tunangoja utaratibu wa uvunaji toka idara ya misitu(W).

**CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO**

- Miti ya Acrocarpus kuharibu mazingira
- Kuna uhaba wa Askari mgambo
- Wazazi wengi kutowalipia watoto wao chakula cha mchana shuleni.

**NAMNA YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO HIZO**

- Orodha ya miti ya Acrocarpus imepelekwa wilayani kwa hatua za uvunaji
- Viongozi wanaelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kujiunga na jeshi la Mgambo .

**MWISHO**

Taarifa hii imeandaliwa na kamati ya maendeleo ya kata ya Msangeni

MH. FIHIRI .H. MVUNGI
MWENYEKITI

LAURENT.A. SIMBA
Kny:AFISA MTENDAJI KATA

AFISA MTENDA.
KATA YA MSANGENI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

OFISI YA AFISA MTENDAJI KATA,
KATA YA LANG'ATA,
S.L.P 176,
MWANGA
03/11/2017

KUMB.NA.K/LANG/MT/6/92
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 176,

MWANGA.

YAH: KUKUTUMIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SAHUGHULI ZA MAENDELEO ROBO YA KWANZA (JULY-SEPTEMBER) 2017 KATIKA KATA YA LANG'ATA

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

Pamoja na taarifa na barua hii nimeambatanisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata ya Lang'ata zilizotekelezwa katika robo hii ( July-September)

Kwa heshima naomba kuwasilisha

AFISA MTENDAJI
KATA YA LANG'ATA

ABDULRAHMAN A. KOMESHA

KAIMU MTENDAJI KATA LANG'ATA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

KATA YA LANG'ATA

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA MAENDELEO KATIKA KATA YA LANG'ATA ROBO YA KWANZA JULAI –SEPTEMBA

## 1. UTANGULIZI

(A) Kata ya Lang'ata ipo katika mwambao wa Bwawa la Nyumba ya Mungu na ni miongoni mwa kata ishirini zianzounda halmashauri ya wilaya ya mwanga.

(B) Miapaka kata ya Lang'ata imepakana na:

- Kasakazini –imepakana na Kata ya Kileo
- Kusini –imepakana na kata ya Kirya
- Mashariki –imepakana na kata ya Mwanga
- Magharibi –imepakana na wilaya ya Moshi vijijini na wilaya ya Simanjiro.

(C) Utawala: Kata hii imeundwa na vijiji vine (4) na vitongoji (12) ambavyo ni:-

| VIJIJI | VITONGOJI |
|---|---|
| HANDENI | Kwa Banda, Mabomani, na Bunge |
| LANG'ATABORA | Kazamwendo, KNCU kati, na Amboni |
| KAGONGO | Lang'ata ndogo, Barafu, Mashine na Kiwanja |
| NYABINDA | Muungano na Jauma |

(D) Elimu: Kata ya Lang'ata ina shule za misingi sita (6) na shule ya sekondari moja (1) ambazo ni:-

i. Shule ya msingi Lang'ata
ii. Shule ya msingi Bwawani
iii. Shule ya msingi Profesa Maghembe
iv. Shule ya msingi Handeni
v. Shule ya msingi Kagonmgo
vi. Shule ya msingi Nyabinda
vii. Shule ya Sekondari Lang'ata bora.

(E) Afya: Kata ya Lang'ata ina kituo cha afya ambacho kipo katika kijiji cha kagongo na zahanati tatu ambazo ni:-

i. Zahanati ya kijiji cha Handeni
ii. Zahanati ya kijiji cha Lang'ata
iii. Zahanati ya kijiji cha Nyabinda

## 2. ULINZI NA USALAMA KATIKA KATA

(A) Kata hii ina mahakama moja iliyopo kijij cha Kagongo na kituo kidogo cha polisi kilichopo katika kituo cha Lang'ata bora

## III. MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HANDENI | | ~~3,411,000~~ | | |
| 2 | LANG'ATA BORA | | 3,411,000 | | |
| 3 | KAGONGO | | 674,000 | | |
| 4 | NYABINDA | | 444,000 | | |

4,529,000 Jumla

## IV. MAPATO YA ICHF

| NA | KIJIJI | ICHF | PAPO KWA PAPO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | HANDENI | - | - | - |
| 2 | LANG'ATA BORA | 1,050,000/= | 132,000/= | 1,182,000/= |
| 3 | KAGONGO | 2,640,000/= | 464,000/= | 3,104,000/= |
| 4 | NYABINDA | - | - | - |

4,286,000/= Jumla

## 5. MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA

(i) Miradi ya maendeleo

(a) Ujenzi wa zahanati katika kijiji cha Lang'ata bora
Mradi huu umefikia hatua ya lenta kwa kipindi hiki

(b) Ujenzi wa wa madarasa mawili shule ya msingi Kagongo
Kuweka milango vyumba vyote viwili, pamoja na sakafu kwenye kordo.

(c) Ujenzi wa ofiasi ya kijiji Nyabinda
Kazi iliyoafanyika ni kufyatua tofali idadi ya 1200

(ii) **TAARIFA ZA KISEKTA (IDARA ZINAZOTOA HUDUMA)**

**(a) MAENDELEO YA JAMII**

Katika idara ya maendeleo ya jamii kazi zilizofanyika ni:

(i) Kutembelea vikundi mbalimbali vya ujasiriamali kwaajilio ya kutoa ushauri na kubadilishana mawazo. Pia kutoa elimu kuhusu mikopo ya wanawake na vijana

**(b) MAZINGIRA**

Shughuli za usafi wa mazingira ni endelevu na zinafatiliwa kwa ukaribu kaya hadi kaya. Pia usimamizi mkubwa umefanyika kwa kushirikiana na viongozi wote katika siku za usafi wa mazingira kitaifa yaani klila jumamosi ya mwisho wa mwezi

**(C) KILIMO NA MIFUGO**

**(C) KILIMO NA MIFUGO**

Kazi zilizofanyika katika idara hii ni kama ifuatavyo ni:-

(i) Mifugo 276 ilitibiwa magonjwa mbalimbali kama homa ya mapafu, minyoo na upungufu wa madini. Ng'ombe 42, mbuzi 58, kondoo 120, nguruwe 30 mbwa 6 na kuku 20 walitibiwa.

(ii) Mifugo 326 iliogeshwa kwa dawa ili kukinga maradhi hasa yaenezwayo na kupe na mbung'o kama ndingana na ndorobo. Mifugo ilioogeshwa ni ng'ombe 126, kondoo 20, mbuzi 110, nguruwe 20,ngamia 8 na kuku 62(walinyunyuziwa dawa –sevin dust)

**(D) ELIMU**

Katika idara hii kazi zilizofanyika katika robo ya kwanza ni kama ifuatavyo:-

(i) Elimu msingi: Mitihani ya kitaifa ya darasa la saba imefanyika

(ii) Elimu sekondar: shule imeweka mikakati ya kuinua taaluma ili kupunguza idadi ya wanafunzi wanaopata daraja la 0

**(E) AFYA**

Kazi zilizofanyika nikama ifuatavyo katika idara hii:-

(i) Usafi wa mazingira ulifanyika kila jumamosi ya mwisho wa mwezi.

(ii) Pia ulifanyika ukaguzi wa majengo ya biashara. Mighahawa 10, maduka 16, na Bar 2

**(D) UVUVI**

OShughuli za uvuvi zimeendelea kufanyika usiku na mchana kama kawiada katika kipindi chote cha miezi mitatu ya robo ya kwanza. Pia uvuvi haramu unaendelea wa kutumia makokoro na vimila unafanyika

Katika idara hii kazi zilizofanyika ni:-

i. Kutolewa elimu elekezi kwa wavuvi pamoja na viongozi wao ili kuona umuhimu wa kuvuva kwa kutumia nyavu zinazokubalika na kuachana na uvuvi wa kutumia makokoro na vimila

ii. Kufanyika doria na kufanikiwa kukamata nyavu moja ya chandarua, kimila kimoja, nyavu za njenga, na nyavu za kokoro mbili.

(iii) Kuimarishwa kwa BMU mbalimbali katika kupambana na uvuvi haramu

**6. CHANGAMOTO NA NAMNA AU MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO KWA UJUMLA.**

**(i) CHANGAMOTO**

(A) Miundombinu ya barabara ni mibovu

(B) Kuendelea kwa uvuvi haramu japokuwa bwawa limefunguliwa.

(C) Upungufu wa watumishi wa uma hasa katika idara ya afya, utawala na elimu

(D) Ukosefu wa maji katika kituo cha afya kagongo.

**(ii) MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO.**

(A) Tunaomba serikali itupatie fungu la kutengeneza barabara

(B) Halmashauri ya wilaya itoe ushirikiano wa kutosha katika kudhibiti uvuvi na uvuvi haramu.

(C) Ajira mpya zitolewe ili kuondoa tatizo la upungufu wa watumishi

(D) Kamati ya maendeleo ya kata imepanga utaratibu wa kukusanya michango kutoka kwa wananchi kwa ajili kununua mabomba na mashine kwa ajili ya kuvutia maji.

**7. MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**

**(I) MAPENDEKEZO**

(A) Watendaji na wataalamu ngazi ya kata wawezeshwe vyombo vya usafiri ili wawafikie wananchi kwa urahisi na kwa wakati

**(iii) HITIMISHO**

Mheshimiwa mwenyekiti, usimamizi wa shughuli za maendeleo unahitaji ushirikishwaji naushirikiano wa kiwango cha juu. Kila mmoja kwa nafasi yake atomize wajibu wake ipasavyo , kwa kuifanya hivyo tutafikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa mwenyekiti naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI                                                  KATIBU

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

## TAARIFA YA KATA YA MWANIKO TAREHE 14/11/2017

### 1. UTANGULIZI

Kata ya Mwaniko imepakana na Kata nyingine nne yaani Kata ya Kifula kwa upande wa Kusini na Kata ya Kivisini na Jipe upande wa wa Mashariki.

### 2. UTAWALA

Kata ya Mwaniko ina vijiji vinne (4) ambavyo ni Mwaniko, Mriti, Mangio na Vuchama-Ngofi. Kata hii ina jumla ya vitongoji 22.

### 3. ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama katika Kata ya Mwaniko ni salama kabisa. Hakuna wageni wowote walioingia katika Kata bila utaratibu na hakuna matukio yoyote ya uvunjifu wa amani yaliyoripotiwa.

### 4. VIKAO VYA KISHERIA NGAZI ZA VITONGOJI, VIJIJI NA KATA

- Kijiji cha Mriti kila kitongoji walipanga kufanya vikao 3 na vyote vilifanyika isipokuwa kitongoji cha Mchombo walifanya vikao 2 ambapo kikao kingine watafanya katikati ya mwezi huu. Pia vikao vya halmashauri ya kijiji vilifanyika 3 na mkutano mkuu maalumu mmoja ulifanyika.
- Kijiji cha Mwaniko kila kitongoji kilipanga kufanya vikao 2 na vyote vilifanyika. Vilevile, kikao 1 cha halmashauri ya kijiji kilifanyika. Kijiji cha Mwaniko hakina mtendaji wa kijiji.
- Kijiji cha Mangio kila kitongoji walipanga kufanya vikao 2 na vyote vilifanyika ila vikao vya halmashauri ya kijiji na mikutano mikuu haijafanyika kwa kuwa hawana mtendaji wa kijiji.
- Kijiji cha Vuchama-Ngofi kila kitongoji kilipanga kufanya vikao 3 na vyote vilifanyika. Pia vikao vya halmashauri ya kijiji vilifanyika 3 na mikutano mikuu 2 ilifanyika kwa kipindi hiki cha miezi mitatu.
- Kata ya Mwaniko ilifanya kikao 1 cha maendeleo ya Kata (WDC) na kikao 1 cha dharura.

### 5. AFYA

Kata ya Mwaniko ina zahanati 3 za serikali ambazo ni Mangio, Mriti na Vuchama.

(i) Mradi wa ujenzi wa zahanati ya Kata ya Mwaniko unaendelea taratibu kwani nguvu za wananchi na wafadhili wamekamilisha msingi wa mzunguko wa nje na kwa ndani. Mnamo mwezi Septemba kijiji kilipata ufadhili wa Tsh 1,400,000/= kutoka kwa mwanakijiji anayeishi nje ya nchi. Fedha ambazo zimeshatumika

mpaka sasa ni Tsh 9,800,000/= . Ili awamu ya kwanza ya ujenzi wa msingi ikamilike makisio yalikuwa 22,600,000/= hivyo bado 12,800,000/= ili kukamilisha awamu ya msingi. Tunazidi kukumbushia kuwa tunaomba mradi huu uingizwe katka bajeti ya halmashauri ya Wilaya ya Mwanga.

(ii) Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Mangio bado unaendelea. Tunazidi kukumbushia msaada wa kuezeka bati kwa vyumba 11 kwa haraka ili kuepusha kuharibika kwa kuta za vyumba hivyo .

(iii) Ujenzi wa choo cha wajawazito katika zahanati ya Vuchama umekamilika. Kila kaya katika kijiji walichangia Tsh 5000/= na jumla ya Tsh 1,496,000/= zimetumika.

(iv) Zahanati ya Mangio inakabiliwa na upungufu wa watumishi ambapo kwa sasa wapo 2 tu. Pia inakabiliwa na tatizo la uchakavu wa majengo, ukosefu wa nyumba za watumishi na sehemu maalum pa kuteketezea taka.

(v) Nyumba ya watumishi katika zahanati ya Mriti inahitaji ukarabati mkubwa. Pia zahanati haina choo cha watumishi.

(vi) Michango ya CHF ni kama ifuatavyo;
- (a) Kjiji cha Mriti wamekusanya jumla ya Tsh 60,000/=
- (b) Kijiji cha Mwaniko wamekusanya Tsh 180,000/=
- (c) Kijiji cha Mangio wamekusanya Tsh 420,000/=
- (d) Kijiji cha Vuchama-Ngofi wamekusanya Tsh 510,000/=

## 6. ELIMU

### (a) Elimu ya msingi

Kata ya mwaniko ina shule za msingi 7 ambazo ni Njuweni,Vuchama, Managugu, Mangio, Mcheni, Chimbi na Mriti.

(i) Shule ya msingi Mriti inakabiliwa na changamoto ya choo cha walimu. Jengo limeshaanzwa kwa nguvu za wananchi ila bado halijakamilika.

(ii) Shule ya msingi Chimbi hawana kabisa nyumba ya walimu jambo linalowapa shida pindi wanapopata watumishi wapya au kutembelewa na wageni.

(iii) Katika shule ya msingi Mangio, chumba cha darasa la awali kimeshajengwa kwa 70% ila bado hakuna fedha za kumalizia. Pia katika shule ya msingi Mangio wanakabiliwa na tatizo la umeme na nyumba za walimu.

(iv) Shule ya msingi ya Njuweni inakabiliwa na ukosefu wa darasa la awali. Tathmini imeshafanyika na inahitajika Tsh 10, 344,600/= ili kukamilika. Utaratibu wa wananchi kuchangia unaendelea.

(v) Shule ya msingi Managugu nayo pia inakabiliwa na ukosefu wa darasa la awali ambapo tathmini inaonesha inahitajika Tsh 12,909,600/=. Wananchi wanajipanga kuanza kuchangia mradi huu.

(vi) Shule ya msingi Vuchama haina mwalimu wa darasa la awali.

(vii) Shule ya msingi ya Mcheni inakabiliwa na uchakavu wa mabati katika ofisi ya walimu na baadhi ya madarasa. Pia ngazi zinahitajika katika maeneo ya shule ili kuepusha mmomonyoko na ajali wakati wa kipindi cha mvua.

**(b) Elimu ya sekondari**

Kata ya Mwaniko ina shule 2 za sekondari za serikali ambazo ni Chaangaja na Ubang'i.

Shule ya sekondari Chaangaja inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

(i) Inakabiliwa na uhaba wa mwalimu mmoja wa hisabati

(ii) Shule hii ina maabara mbili za Kemia na Bayolojia ambazo hata hivyo hazijakamilika vizuri. Pia shule haina kabisa maabara ya somo la Fizikia.

(iii) Vilevile, shule hii inakabiliwa na uchakavu mkubwa wa madarasa hasa yale yaliyorithiwa kutoka shule ya msingi Chimbi ambapo yanahitaji ukarabati mkubwa. Pia 60% ya vyoo vya wanafunzi katika shule hii ni vya kizamani ambapo havifai kwa matumizi ya sasa kiafya. Shule hii pia ina nyumba ya mwalimu moja tu tofauti na mahitaji halisi.

(iv) Kutokana na Jiografia ya eneo la shule hii kunahitajika ujenzi wa ngazi katika maeneo mbalimbali ya shule ili kuepusha ajali kwa walimu na wanafunzi hasa kipindi cha mvua.

Shule ya sekondari Ubang'i inakabiliwa na changamoto zifuatazo;

(i) Lipo jengo la nyumba ya mwalimu lakini bado halijakamilika. Tathmini inaonesha kuwa bado Tsh 30,000,000/= ili liweze kukamilika.

(ii) Kuna ujenzi wa darasa moja ambao bado unaendelea. Bado inahitajika Tsh 7,000,000/= kukamilisha ujenzi huo.

(iii) Jengo la maabara ujenzi umeanza ila bado tathmini itafanyika ili kujua kiasi kinachohitajika ili kukamilisha ujenzi huo.

(iv) Shule hii pia haina mwalimu wa hesabu.

## 7. MAPATO YA HALMASHAURI

(a) Ada za leseni

- Vuchama-Ngofi wamekusanya 75,000/=
- Mriti wamekusanya Tsh 50,000/=
- Mwaniko taarifa hazijakamilika.
- Mangio bado taarifa zilikuwa hazijakamilika.

(b) Mapato ya ushuru wa ukaguzi wa nyama kwa ujumla Tsh 90,000/= zimekusanywa kwa Kata nzima.

- ✓ **Changamoto** inayokabili ukaguzi wa nyama ni kutokuwepo kwa mihuri ya kupiga nyama mara baada ya kukagua.

## 8. MIRADI MINGINE KATIKA KATA

(a) Mradi wa ofisi ya kijiji cha Mriti umekamilika kwa 85% .bado Tsh 3,476,000/= ili kukamilisha ujenzi.

(b) Mradi wa barabara ya kutokea Mriti hadi Kambi ya Simba bado unaendelea . Makisio katika barabara hii yalikuwa Tsh 60,000,000/= ili iweze kupitika kwa pikipiki. Tayari Tsh 37,000,000/= zimeshatumika kupitia nguvu za wananchi,wafadhili mbalimbali na mfuko wa Jimbo. Hata hivyo mnamo mwezi Oktoba kijiji kilifanya tamasha na kupata Tsh 2,500,000/= ambapo taslimu ilikuwa Tsh 1,600,000 na ahadi ni Tsh 900,000/= Bado Tsh 20,500,000 ili barabara hii iweze kukamilika.

(c) Mradi wa uchimbaji wa maji wa visima vikubwa umeshafanyika kwa kijiji cha Mwaniko kinachosubiriwa kwa sasa ni timu ya tathmini kwa ajili ya usambazaji wa maji hayo. Kwa vijiji vya Mriti na Mangio upimaji ulishafanyika lakini bado uchimbaji haujaanza.

(d) Mradi wa ofisi ya kijiji cha Mwaniko ambao unajengwa kwa ruzuku na nguvu za wananchi nao bado haujakamilika kwa 100%. Bado inahitajika Tsh 2,700,000/= ili uweze kukamilika.

(e) Mradi wa vitambulisho vya Taifa unaendelea kwa sasa katika Kata nzima ya Mwaniko kwa wananchi kujaza form.

(f) Mradi wa barabara kutoka Mwaniko kupitia Sechuni hadi Mchombo umefanyika kwa nguvu za wananchi.

## 9. UCHUMI

Hali ya chakula katika Kata ya Mwaniko si mbaya sana kwani asilimia kubwa ya wakulima walipata mavuno ya kutosha kwa msimu wa masika. Tunaendelea kuhamasisha wananchi kutumia vizuri chakula na kutumia mbegu bora kwa ajili ya msimu ujao. Katika vijiji vyote upandaji wa mbegu mpya za kahawa, maparachichi na vanilla unaendelea kwa kutumia mvua za vuli.

- ✓ **Changamoto** iliyopo katika Kata ya Mwaniko ni uharibifu wa mazao unaosababishwa na wanyama wa mwituni kama tumbili, kima na nyani. Tunaomba ofisi ya maliasili Wilaya ya Mwanga itusaidie katika kupambana na wanyama hawa.
- ✓ Pia wakulima wa Kata ya mwaniko wanaomba wapewe bembejeo za kilimo ili waweze kulima kilimo bora na kuongeza tija katika uzalishaji.

## 10. MAZINGIRA

Katika Kata ya Mwaniko usafi wa mazingira unafanyika vizuri katika kila kijiji kutokana na utaratibu waliojiwekea. Vilevile, kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi usafi hufanyika

kwa kuwahusisha wananchi wote kama ambavyo Mheshimiwa Rais alivyoagiza,Pia ulinzi wa vyanzo vya maji umeimarishwa na wananchi wameendelea kuhamasishwa kuhusu athari za kufanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.

- ✓ **Changamoto** katika suala la mazingira ni miti ambayo si rafiki wa vyanzo vya maji. Ofisi ya maliasili imetuma barua ya kuitambua miti hiyo katika vijiji vyetu lakini bado haijatoa muongozo namna ya kuikata miti hiyo ili kuepusha mkanganyiko wa kisheria.

-MWISHO-

IMEANDALIWA NA,

| | |
|---|---|
| ………………………………… | ………………………………… AFISA MTENDAJI KATA YA MWANIKO |
| BARAKA AMIRI MARADONA | NECHI ANDERSON MOSHI |
| **DIWANI KATA YA MWANIKO** | **AFISA MTENDAJI KATA YA MWANIKO** |

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO ZA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2017/2018 JULAI-SEPT KATA YA KIRONGWE

1. **UTANGULIZI**

Kipindi hiki cha kuanzia mwezi Julai hadi mwezi Septemba kilikuwa ni kipindi cha maandalizi ya mashamba kwa ajili ya mvua za vuli kama wakulima walivyo kuwa wakihamasishwa na maafisa Ugani.

2. **ULINZI NA USALAMA**

Hali kwa ujumla ilikuwa shwari ila matukio madogo madogo yaliyo jitokeza yalishughulikiwa katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata na Mahakama. Kwa mfano kesi ya madai na wizi wa kuku.

3. **VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA**

Baadhi ya vijiji kati ya vijij 5 katika Kata ya Kirongwe vilifanikiwa kufanya vikao vyote vya Halimashauri kwa mujibu wa sheria ~~na~~ ila mikutano mikuu. ~~Aidha~~ vijiji vingine vilishindwa kutokana na changamoto ya ukosefu wa Maafisa watendaji katika vijiji husika.

Pia kuna changamoto ya kutokufanyika mikutano ya vitongoji kama jedwali linavyoonesha hapo chini, kama ifuatavyo:-

**VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA**

| KIJIJI | IDADI YA VIKAO VYA HALIMASHAURI | IDADI YA MIKUTANO MIKUU | IDADI YA MIKUTANO YA VITONGOJI |
|---|---|---|---|
| 1. MWERO | 3 | 1 | 0 |
| 2. VUAGHA | 3 | 1 | 5 |
| 3. MBORE | 3 | Uliahirishwa | 0 |
| 4. LOMWE | 2 | 0 | 2 |
| 5. KIRICHE | 1 | 0 | 0 |

4. **MAPATO JULAI – SEPTEMBER** – 2017.

| AINA YA MAPATO | KIASI KILICHOKUSANYWA | | |
|---|---|---|---|
| | JULAI | AUGUST | SEPTEMBER |
| UKAGUZI WA NYAMA | 92,200/= | 77,200/= | 100,300/= |

**JUMLA YOTE NI 269, 700/=**

5. **TASAF**

| KIJIJI | WALENGWA | KIASI POKELEWA |
|---|---|---|
| LOMWE | 24 | 692,000/= |
| VUAGHA | 13 | 420,000/= |
| KIRICHE | 16 | 480,000/= |
| MBORE | 61 | 181,600/= |
| JUMLA | | 1,773,600/= |

6. Jumla ~~**JUMLA**~~ **ZAWATUMIA MAJI**:-

| KIJIJI | MAPATO | MATUMIZI | BENKI |
|---|---|---|---|
| KIRICHE & MWERO | 1,041,392/= | 610,800/= | 430,592/= |
| VUAGHA | 1,035,977.14 | 299,300/= | 736,677.14 |
| LOMWE | 339,998.30 | 190,500/= | 149,498.30 |
| | 2,417,367.44 | 1,100,600/= | 1,316,767.44 |

7. **TAARIFA ZA KISEKTA**

(i) **ELIMU**

Kata ya Kirongwe ina shule za msingi 6 na sekondari 1. Katika shule za msingi 6 zilipaswa kuwa na walimu 54 lakini kuna walimu 33 na upungufu wa walimu ni 21 na sekondari ina walimu 40 ambao wanajitosheleza.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO NYINGINE**

1. Kuna ukosefu wa walinzi mashule kati ya 6 shule zenyewe walinzi ni 2 tu katika shule za msingi Kata ya Kirongwe.
2. Bado kuna ukosefu wa chakula cha mchana mashuleni.
3. Uchakavu wa miundo mbinu katika shule za msingi na sekondari bado upo.

(ii) **MAJI**

Wananchi wanapata maji kwa zamu kulingana na taratibu zilizowekwa na jumuiya zao. Changamoto zilizojitokeza kwa kipindi hiki ni upungufu wa maji kutokana na ukame wa muda mrefu.

(iii) **KILIMO NA USHIRIKA**

Kwa upande wa kilimo, kilikuwa ni kipindi cha uhamasishaji wa maandalizi ya mashamba sambamba na uoteshaji wa migomba kabla ya mvua za msimu wa vuli kuanza.

Changamoto iliyopo ni ukosefu wa pembejeo za kilimo hasa mbegu na endapo zikipatikana wakulima ~~wanazipata~~ wazipate kwa bei ~~ghali~~ rafiki, badala ya ghali.

(iv) **MIFUGO**

Huduma za matibabu na ushauri kwa kipindi hiki zilitolewa japo kuna changamoto ya ukosefu wa Afisa mifugo wa Kata na vijiji.

(v) **AFYA**

Uhamasishaji wa bima iliyo boreshwa na ulipiaji wake unaendelea kutolewa ~~kwa~~ kwa wananchi kupitia wahudumu wa Afya ~~wanatoka~~ kwenye vitongoji vilivyomo ndani ya Kata ya Kirongwe.

Na elimu mbalimbali zinaendelea kutolewa kwa wananchi namna gani waweze kuepukana na magonjwa ~~ikiwa ni kunawa mikono~~ ya aina zote. ICHF haikupatikana itatolewa robo ijayo.

(vi) **MIUNDO MBINU** :-

Barabara za vitongoji katika Kata ya Kirongwe wananchi wanaendelea kuzihudumia kupitia misaragambo. Urefu wa 1 Km umechimbwa ktk robo hii ya kwanza ya mwaka 2017/18.

**CHANGAMOTO MBALIMBALI**

(1) Kutokana na hali duni ya kipato cha wananchi wameshindwa kukamilisha kwa wakati miradi walio ibua vijijini, mfano ujenzi wa majengo ya Ofisi ~~kwa~~ za kijiji cha Lomwe, (Mbore, ukumbi wa mikutano) Mwero, endelezo la ujenzi wa ofisi ya kijiji cha hicho lipo.

Changamoto nyingine ni kuchakaa kwa Ofisi ya Kata ya Kirongwe licha ya uchakavu eneo iliyo ofisi ni barabarani sana na kutokana na ujenzi wa barabara unaoendelea imekuwa adha kubwa sana.

(2) Ukosefu wa V.E.O. vijiji vya Mbore, Lomwe na Kiriche.

Naomba kuwasilisha taarifa hii.

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| MWENYEKITI | KATIBU |
| 1/11/2017 | 1/11/2017 |
| AMIRI MKONDO SARUMBO | FARIDA MPOGOLO. |

AFISA MTENDAJI
KATA YA KIRONGWE

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA.**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATA YA KIGONIGONI ROBO YA KWANZA JULAI MPAKA SEPTEMBA.**

1. **UTANGULIZI.**
   i. **MIPAKA:** Kata ya Kigonigoni ipo tarafa ya Jipendea mashariki inapakana na chi ya Kenya ikitenganishwa na ziwa Jipe. Upande wa mashariki inapakana na kata ya Kwakoa, upande wa magharibi inapakana na kata ya Kirongwe na upande wa kaskazini inapakana na kata ya Jipe.
   ii. **UTAWALA**: Kata hii inaundwa na vijiji vinne(4) vya Kigonigoni, Kwakihindi, Butu Usangi na Ruru na pia inajumla ya vitongoji nane (8) kila kijiji vitongoji viwili(2).
   iii. **ELIMU**: Kata hii ina shule za msingi tatu(3) ambazo ni shule ya msingi Kigonogoni, shule ya msingi Kwakihindi na shule ya msingi Ruru. Pia kata hii ina shule ya sekondari ambayo ni shule ya sekondari Kigonigoni.
   iv. AFYA:Kata hii ina kituo kimoja cha afya cha Kigonigoni.
   v. **NJIA KUU ZA UCHUMI**: Wananchi wa kata hii wanategemea kilimo, ufugaji na uvuvi kama njia kuu ya kuwaingizia kipato.

2. **ULINZI NA USALAMA KATIKA KATA.**
   Hali ya ulinzi na usalama katika kata ni shwari.

3. **VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA, VIJIJI NA VITONGOJI.**

**i). KIKAO CHA WDC/KMK.**

| NA | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGONIGONI | 1 | 1 | |

ii).**VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI.**

| NA | KATA | KIJIJI | VIKAO | | MKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| 1 | KIGONIGONI | KIGONIGONI | 3 | 2 | 1 | 1 | |
| | | BUTU USANGI | 3 | 1 | 1 | 1 | |
| | | KWAKIHINDI | 4 | 2 | 1 | 1 | |
| | | RURU | 3 | 1 | 1 | 1 | |

**iii). MIKUTANO YA WAKAZI WA VITONGOJI.**

| NA | KATA | KIJIJI | JINA LA KITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGONIGONI | KIGONIGONI | KIGONIGONI A<br>KIGONIGONI B. | 3<br>3 | 2<br>1 | |
| | | BUTU USANGI | MGWELO<br>SOKONI | 3<br>4 | 1<br>2 | |
| | | KWAKIHINDI | KWAKIHINDI A<br>KWAKIHINDI B | 3<br>4 | 1<br>2 | |
| | | RURU | RURU A<br>RURU B | 4<br>3 | 1<br>2 | |

4. **MAPATO NA MATUMIZI.**

i. **TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI ZILISOMWA KWENYE MIKUTANO MIKUU YA VIJIJI.**

Katika kipindi cha robo ya kwanza, taarifa za mapato na matumizi zilisomwa na kukubaliwa kwenye mikutano mikuu ya vijiji vya kata ya Kigonigoni kama ifuatavyo;

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGNEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGONIGONI | 1 | 1 | |
| 2. | BUTU USANGI | 1 | 1 | |
| 3. | KWAKIHINDI | 1 | 1 | |
| 4. | RURU | 1 | 1 | |

ii) **MAPATO YA HALIMASHAURI YA WILAYA.**

Katika kipindi cha robo ya kwanza, vijiji vya kata hii vilikusanya mapato ya Halmashauri ya wilaya kama inavyoonekana hapa chini.

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGNEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGONIGONI | 100000. | 0 | 0% | |
| 2. | BUTU USANGI | 140000 | 60000 | 42.85% | |
| 3. | KWAKIHINDI | 100000 | 110000 | 110% | |
| 4. | RURU | 100000 | 0 | 0% | |

iii). **MAPATO YA HALMASHAURI YA KIJIJI.**

Mapato ya halmashauri za vijiji katika kata ya Kigonigoni yalikuwa kama ifuatavyo;

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGNEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGONIGONI | 100000. | 0 | 0% | |
| 2. | BUTU USANGI | 150000 | 0 | 0% | |
| 3. | KWAKIHINDI | 100000 | 0 | 0% | |
| 4. | RURU | 160000 | 0 | 0% | |

5. **TAARIFA ZA KISEKTA NA MIRADI YA MAENDELEO.**

**TAARIFA ZA KISEKTA.**

i. **SEKTA YA ELIMU;**

**Shule ya sekondari Kigonigoni.**

a) Mradi wa maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi unaendelea vizuri kwani jengo limeshawekwa umeme ( wiring) na fundi pamoja na mzabuni wameshalipwa fedha kwa hatua waliyoifikia.

b) Mradi wa bweni la wanafunzi; mradi huu upo katika hatua za awali kwani mpaka sasa tumefanikiwa kupata jumla ya tofali zilizochomwa elfu nane (8000), ikiwa ni uwiano wa tofali elfu mbili (2000) kwa kila kijiji katika kata ya Kigonigoni.

c) Bado kuna upungufu mkubwa wa walimu haswa katika masomo ya sayansi na hisabati.
d) Upungufu wa nyumba za walimu.

**Shule ya msingi Ruru.**

a) Mradi wa shimo la choo cha wanafunzi unaendelea vizuri kwani shimo hilo lipo katika hatua ya kujengewa kwa mawe. Vilevile michango inaendelea kutolewa ili kufanikisha mradi huo.
b) Upungufu wa walimu pia ni changamoto kubwa inayoikabili shule hii.

**Shule ya msingi Kwakihindi.**

a. Mradi wa nyumba ya mwalimu unaendelea vizuri na zoezi la michango kwa wananchi limefikia ~~kikomo~~ hivyo fedha zilizopatikana zitatumika kuendeleza mradi huo. DHAMANI YA MRADI 480000
b. Upungufu wa walimu pia ni changamoto kubwa inayoikabili shule hii.

**Shule ya msingi Kigonigoni.**

a) Mradi wa ukarabati wa nyumba ya mwalimu unaendelea vizuri kwani mheshimiwa Diwani ametafuta fungu kwa ajili ya ukarabati huo.

ii. **SEKTA YA KILIMO NA UFUGAJI.**

a) Kutokana na uhamasishaji wa bibi shamba juu ya pembejeo bora za kilimo zaidi ya kilogramu 300 za pembejeo hizo zimeuzwa kwa wananchi katika kata ya Kigonigoni.
b) Katika utekelezaji wa kilimo cha zao la korosho zaidi ya mashimo mia sita (600) yamechimbwa na mashimo 322 kati ya hayo yameshapandwa korosho.
c) Wananchi wanazidi kuhimizwa kupanda mazao yanayoendana na jiografia ya eneo letu na mabadiliko ya hali ya hewa kwa matokeo bora.

iii. **SEKTA YA AFYA**

a. Hakuna magonjwa ya mlipuko yaliyojitokeza hadi sasa
b. Dawa muhimu zinapatikana
c. Bado tunaendelea kuwahamasisha wananchi kujiunga na mfuko wa jamii ulioboreshwa (ICHF)

NAWASILISHA

| | |
|---|---|
| ………………………… | ………………………… |
| JEREMIA A. SHAYO | KIWIA EMANUEL |
| MWENYEKITI | KATIBU |

## KATA YA MWANGA (MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA)

**Mh.Mwenyekiti Halmashauri ya (W) Mwanga.**

**YAH: TAARIFA YA UTEKELEZAJI ROBO YA KWANZA YA MWAKA KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA TAREHE 14/11/2017**

### UTANGULIZI

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga ni miongoni mwa Mamlaka za Miji Midogo zinazoundwa chini ya sheria ya Serikali za mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982 na sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Namba 8 ya mwaka 1982.Mamlaka za Miji Midogo ni Mamlaka zinazojitegemea kisheria na sio sehemu ya Halmashauri ya Wilaya. Mji Mdogo wa Mwanga una eneo la kilometa za mraba 63 upo katika uwanda wa chini ukiwa katikati ya Wilaya ya Mwanga. Mji wa Mwanga unapakana na Kata ya Kileo kwa upande wa Kaskazini. Kata ya Lembeni kwa upande wa Kusini Mashariki , Upande Kusini Magharibi inapakana na Kata ya Lang,ata na upande wa Kaskazini Mashariki unapakana na Kata ya Shighatini.

Kiutawala Mamlaka ya Mji Mdogo imeundwa na Vitongoji 12 vyenye jumla ya watu 15,783 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Mamlaka ya Mji Mdogo imeendelea kuimarisha utawala bora kwa kuhakikisha kwamba shughuli zinaendeshwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu za kidemokrasia.

### HALI YA ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama katika mji wetu ni shwari, wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za kujiongezea kipato kwa amani na utulivu. Aidha jamii ikishirikiana na vyombo vya dola vipo imara kukabili matukio machache ya kihalifu yanayojitokeza, udokozi, wizi na uharibifu wa maliasili zetu na wazururaji walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa hatua za kisheria.

**VIKAO NA MIKUTANO KISHERIA NGAZI YA MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA**

Taarifa ya vikao na mikutano ya kisheria kwa mfumo wa majendwali

**JEDWALI "A" MKUTANO WA BARAZA LA MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA**

| NA | MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MWANGA | 1 | 1 | |

**JEDWALI "B" VIKAO VYA KAMATI ZA KUDUMU MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA**

| NA | MAMLAKA YA MJI MDOGO | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| | Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Miji | 3 | 3 | |
| | Kamati ya Elimu, Afya na Maji | 1 | 1 | |
| | Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira | 1 | 1 | |

**JEDWALI "C" MIKUTANO YA WAKAZI MAMLAKA YA MJI MDOGO MWANGA**

| NA | MAMLAKA YA MJI MDOGO | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Reli Juu | 3 | 1 | |
| 2 | Reli Chini | 3 | 2 | |
| 3 | Mikameni | 3 | 1 | |
| 4 | Mtalang'a | 3 | 3 | |
| 5 | Vudoi | 3 | 2 | |
| 6 | Mwangondi | 3 | 1 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Mikuyuni | 3 | 1 | |
| 8 | Lwami | 3 | 1 | |
| 9 | Mandaka | 3 | 2 | |
| 10 | Kisangiro | 3 | 2 | |
| 11 | Mforo | 3 | 2 | |
| 12 | Kichangare | 3 | 1 | |

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### ELIMU

Tatizo la choo katika shule ya sekondari Vudoi limetatuliwa kwa asilimia kubwa kwani imefanikiwa kujenga choo chenye thamani ya Tsh. 19,000,000/=. Pia shule zote za Sekondari zinaendelea kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapatiwa chakula cha mchana pamoja na shule za msingi.

#### CHANGAMOTO

Idadi ndogo ya wanafunzi wanaochangia kula chakula cha mchana, miundo mbinu mibovu ya shule za msingi kama vyoo - shule ya msingi Mwanga, S/Msingi Lwami na Kisangiro,kwamavusha na shule ya msingi Mandaka.

### MIKAKATI

- Kuwaelimisha wananchi juu ya uelewa wa dhana ya elimu bure ili waweze kutekeleza wajibu wao wa kuchangia gharama za chakula cha mchana na kurekebisha miundo mbinu ya shule.

### MAJI MJINI

Katika kufikia robo ya kwanza 2017/18 Mamlaka ya Maji mjini ilizalisha mita za ujazo 125,903m³ ambapo lengo lilikuwa ni kuzalisha wastani wa 240,240m³ hii ni sawa na asilimia 52% ya lengo tulilojiwekea.

**CHANGAMOTO**

- Tatizo la umeme kukatwa mara kwa mara kwa na TANESCO kwa sababu ya deni la Tsh.200,700,696.20.
- Visima kupunguza uwezo wa kuzalisha kwa sababu ya mabadilikoya tabia nchi.

**MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO**

- Deni limewasilishwa TANESCO kwa ajili ya kulipwa

**AFYA**

**TAARIFA YA iCHF NA PAPO KWA PAPO**

**JULAI - 2017**

Mfuko wa iCHF jumla ya wanachama 127

Kwa mwezi Julai 2017 tumepokea Tsh. 43,333.333/= kutoka iCHF

Papo kwa papo jumla ya wananchama 127 - Tsh 1,016,000/=

**Jumla Tsh. 1,059,333.33**

**AUGOST 2017**

Mfuko wa iCHF jumla ya wanachama 80

Kwa mwezi Augost 2017 tumepokea Tsh. 35,000/=

Papo kwa papo jumla ya wananchama 98 - Tsh 784,000/=

**Jumla Tsh. 819,000/=**

**SEPTEMBA 2017**

Mfuko wa iCHF jumla ya wanachama 212

Kwa mwezi Septemba tumepokea Tsh.176,666.67/=

Papo kwa papo jumla ya wananchama 107 - Tsh 856,000/=

**Jumla Tsh. 1.032,666.67**

**JUMLA KUU TSH. 2,911,000/=**

**TAARIFA YA UJENZI WA WODI YA WAZAZI MWANGA H/C**

- Jengo la wodi ya kina Mama kituo cha Afya Mwanga unaendelea kupitia michango mbali mbali ya serikali na wafadhili mbali mbali na kwa sasa ujenzi huu upo katika hatua ya ukamilishaji.

**KILIMO/MIFUGO**

**MIFUGO**

Wafugaji 119 walitembelewa na kupewa ushauri

**USHAURI ULIOTOLEWA**

- Kutoa chanjo za minyoo kila baada ya miezi mitatu (3)
- Umuhimu wa kuboresha koosafu za mifugo kwa kutumia madume bora
- Kujiunga katika vikundi vidogo vidogo ili kupata unafuu wa kununua madawa
- Kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo yao ili kuwa na uwiano kati ya mifugo na rasilimali zilizopo.

**MIFUGO ILIYOUGUA NA KUPATIWA TIBA**

- Ng'ombe 17
- Mbuzi na kondoo 52
- Kuku 63

**AINA YA MAGONJWA YALIYOJITOKEZA**

- Ndigana kali
- Ndigana baridi
- Ndui ya kuku
- Fowly typhod
- Pnemonia

**CHANGAMOTO**

- Uhaba wa malisho
- Uhaba wa maji
- Magonjwa yanayosababishwa na kupe kwa gharama za dawa
- Kucheleweshwa kwa taarifa kwa maafisa ugani pale wafugaji wanapopatwa na shida za magojwa kwa mifugo yao.

**MIKAKATI**

- Kuwashauri wafugaji kujiunga kwenye vikundi vidogo vidogo ili kupata unafuu wa dawa pamoja na kuhudumiwa kwa urahisi na maafisa ugani.

- Kuendelea kuwashauri wafugaji kutoa taarifa mapema kwa maafisa ugani pale wanapopatwa na shida.
- Kuendelea kuwashawishi wafugaji kuvuna mifugo yao ili kuwa na uwiano kati ya mifugo yao na rasilimali zilizopo

**KILIMO CHA MSIMU WA MASIKA 2017**

Wakulima waliopata ushauri kwa vitongoji 12 ni 219.

Baada ya wakulima kupata ushauri baadhi ya wakulima wamepokea ushauri na kupanda mazao yanayostahimili ukame mfano choroko,kunde na fiwi na korosho na pia baadhi ya wakulima wanaopanda mahindi wamepanda mbegu bora kama vile STUKA ,SEEDCO na DK.

**CHANGAMOTO**

1. Ukosefu wa vyombo vya usafi ili kufika maeneo mbali mbali kwa wakati
2. Uhaba wa mvua wa mara kwa mara
3. Bei kubwa ya pembejeo za kilimo ukilinganisha na uwezo mdogo wa kifedha kwa wakulima.

**MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

- Kushauri wakulima kujiunga katika vikundi ili waweze kununua pembejeo kwa pamoja.
- Kushauri wakulima kupanda mazao yanayostahimili ukame mfano choroko, mtama, kunde, korosho na fiwi.
- Kushauri wakulima wafugaji kuuza mifugo yao ikiwa na afya nzuri ili waweze kujipatia fedha kwa ajili ya kujinunulia chakula
- Kushauri wakulima kutumia chakula kidogo kinachopatikana kwa uangalifu mkubwa ili kuepuka njaa.

**Mazingira**

Zoezi la usafi wa mazingira limekuwa likitekelezwa kila mwisho wa mwezi kwa kufanya usafi kwenye maeneo ya kaya na maeneo ya wazi .

**CHANGAMOTO**

- Baadhi ya wananchi wanapewa maagizo ya afya lakini wanaendelea kutupa taka ovyo mitaani.
- Uchomaji taka kwenye mifereji ya kupitishia maji machafu.
- Baadhi ya wafugaji wanaachia mifugo yao na kuzurura ovyo.

- Ukataji wa miti kiholela unaoendelea kwa baadhi ya maeneo na ufyatuaji wa matofali.
- Uchotaji wa mchanga unaoendelea katika makorongo

**MIKAKATI**

- Wanaoendelea kukaidi maagizo ya usafi na uharibifu wa mazingira wanatozwa faini na wengine kupewa kazi za mikono kama sehemu ya elimu na fundisho.
- Elimu ya utunzaji wa mazingira inaendelea kutolewa kwa wananchi.
- Mifugo inayozurura inaendelea kukamatwa na kutozwa faini kwa kushirikiana na migambo wa ndani na wa nje ya Mamlaka ya Mji Mdogo Mwanga.

**MAPATO**

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga katika kipindi cha Julai hadi Septemba,2017 imekusanya Tsh 31,364,209.61 ya lengo lake la kukusanya Tsh 138,678,000/= sawa na asilimia 34.32 katika mapato yake ya vyanzo vya ndani.

**MATUMIZI**

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga katika kipindi cha Julai hadi Septemba,2017 imetumia Tsh.22,676,290/=

**CHANGAMOTO.**

- Baadhi ya wafanyabiashara kutolipa fedha za leseni kwa wakati.
- Mabadiliko ya utoaji wa leseni kwa kutumia fomu za Tax Clearance ambapo baadhi ya wafanyabiashara hawajaelewa vizuri lengo lake,hivyo hali hii huchangia kuchelewesha zoezi la utoaji wa leseni kwa wakati.
- Kucheleweshwa kwa Fedha za mamlaka Katika Akaunti ya pamoja Kwenda A/C za Mamlaka.

**MIKAKATI**

- Kutoa elimu na ufuwatiliaji wa karibu kwa Wafanyabiashara ili kulipa leseni kwa wakati.

Nawasilisha

..................                                    ......................

***H.M.Mfinanga***

***Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu***

***Mamlaka ya Mji Mdogo Mwanga***

***Mh. Salimu Marijani***

***Diwani Kata ya Mwanga***

***Mamlaka ya Mji Mdogo Mwanga***

AFISA MTENDAJI MKUU
MAMLAKA YA MJI MDOGO - MWANGA
SLP 176 MWANGA

# 1. HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATA YA KILOMENI KWA KIPINDI CHA ROBO MWAKA

## JULY – SEPTEMBER 2017

2. (i) **UTANGULIZI** -Kata ya Kilomeni imepakana na kata ya Lembeni, Kwakoa, Chomvu na ngujini

   (ii) **UTAWALA**-Kata hii ina vijiji viwili (2) ambavyo ni Kilomeni na Sofe

Kuna jumla ya vitongoji 16. Vitongoji 10 vya kijiji cha Kilomeni na vitongoji 6 vya kijiji cha Sofe

(iii) **ELIMU**-Kata ina jumla ya shule nne (4) za msingi ambazo ni kilomeni, sofe, shighatini na Mlevyo kuna shule za secondary mbili (2). Shule ya secondary Maghare, shule ya kata na shule ya secondari ya wasichana Kilomeni ni shule binafsi ya kanisa katholiki

(iv) **AFYA**-Kata ina zahanati mbili (2) moja ya kata na moja ya misheni kanisa katholiki

(iv) **NJIA KUU ZA UCHUMI** -Wananchi wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage, ndizi na miwa. Upo pia ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku. Shughuli za kibiashara ni machuka madogo madogo.

Shughuli zote hizo zinafanyika kienyeji ( Small Scale Agriculture) ni kwa ajili ya matumizi ya chakula tu.

3. **ULINZI NA USALAMA**.

Kwa robo hii ya mwaka hali ya ulinzi na usalama ni shwari. Vilikuwepo vitendo vichache vya kihalifu vilivyoendelea kuonekana kama uvutaji wa bangi, ulevi na wizi wa mazao shambani.

Hatua zilizo chukuliwa

I. Wananchi waliendelea kuelimishwa athari za matumiza ya madawa ya kulevye kupitia mikutano ya vitongoji na vijiji

II. Walioonekana ~~wakiporomosha~~ Kutoa matusi ~~au~~ kwa sababu ya ulevi au vinginevyo walikamatwa na kushitakiwa katika baraza la kata na walipokutwa na hatia kwa mujibu wa sheria ndogo za serikali za mitaa waliadhibiwa kwa kupigwa faini. ~~Kutoka (ULINZI NA USALAMA Hatua zilizochukuliwa)~~

III. Tumeanzisha mafunzo ya jeshi na akiba, vijana wapatao, 86 wamejiunga na mafunzo hayo na tayari mkuu wa wilaya amefungua mafunzo hayo tunamshukuru. japo walijabaki 57

IV. Mkuu wa wilaya aliongea na wananchi katika mkutano wa hadhara na kusikiliza kero za wananchi na kupatikana ufumbuzi wa kero hizo za wananchi na kupatikana kwa njia hii wananchi walijisikia huru na salama zaidi.

V. Kumeanzishwa mikakati ya ujenzi wa kituo cha Polisi ili kukabiliana na wimbi la uharibifu na uvunjifu wa amani ili wananchi waweze kuwa salama zaidi.

V: Lipo tukio la mtoto kupotea ...

4. SEHEMU YA NNE
VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA, VIJIJI NA VITONGOJI

(i) JEDWALI "A" VIKAO VYA WDC /KMK

| NA | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KILOMENI | 1 | 1 | |

NN (ii) JEDWALI "B" VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA KIJIJI

| No. | KATA | | VIKAO | | MKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KILOMENI | KIJIJI | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| | | KILOMENI | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | SOFE | 3 | 2 | 1 | 1 | |

MIKUTANO YA VITONGOJI

| No. | KATA | KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | KILOMENI | KILOMENI | 10 | 30 | 13 | [illegible] |
| | | SOFE | 6 | 18 | 6 | [illegible] |

5. SEHEMU YA TANO
MAPATO NA MATUMIZI YALIYOSOMWA.

| No. | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KILOMENI | 1 | 1 | |
| 2. | SOFE | 1 | 1 | |

MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA-

| No. | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KILOMENI | – | 255,000 | |
| 2. | SOFE | – | 153,000 | |
| 3 | NYAMA | 54,000 | 67,500 | |

JUMLA = 475,500/=

(iii) MAPATO YA HALMASHAURI ZA VIJIJI

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilomeni | | 1,220,000 | | |
| 2 | Sofe | | ~~1,962,500~~ 2,446,500 | | |
| | JUMLA TSH. | | 3,182500 | | |

## 6.MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA

### A. MIRADI YA MAENDELEO.

Miradi inayoendelea kutekelezwa ni:-

**I. Miradi wa maji ya bomba**

Mradi huu uko katika hatua za mwisho mwisho kipindi hiki wananchi na viongozi wa kata na vijiji wanaendelea kubaini mapungufu ya kuifundi ya mradi huo na kumjulisha mhandisi wa maji wilaya kumjulisha mkandarasi kwa ajili ya marekebisho.

Hadi sasa marekebisho kadhaa yamekwisha kufanywa na yanaendelea kufanywa ili mradi ukamilike na kukabidhiwa kwa wananchi.

II. Mradi wa bara bara ya kutoka kisekibaha Kilomeni. Wananchi wameendelea kuboresha bara bara hiyo kwa njia ya misaragambo na tamasha

III. Mradi wa chumba cha maabara shule ya sekondari maghare mradi huu upo katika hatua za upauaji ; mbao ni nguvu za wananchi na mabati tumeomba kwa mkurugenzi mtendaji kama nguvu za Halmashauri, bado mabati hayajapatikana.

IV. Zahanati ya kata: vyumba viwili kwa ajili ya kulaza wagonjwa, viko katika hatua ya plasta, madirisha, milango, sakafu na rangi, = Bado.

V. Wananchi wamekubaliana kuchanga pesa kwa ajili ya kuendeleza mradi huu ambao awali ulikuwa unaendeshwa na wahisani na kurudishwa kwa wananchi baada ya hali yao ya kifedha kukwama-juhudi za kutafuta wahisani wengine zinashughulikiwa na viongozi wa kata ikiwa ni pamoja na kuomba halmashauri vifaa vya viwandani.

VI. Mradi wa ujenzi wa ofisi ya kijiji cha sofe. Yamegawiwa kwa vitongoji vya kijiji hiki na wanatazamiwa kukabidhi matofali hayo na mawe ili ujenzi uanze kunako mwezi November 2017

VII. Ujenzi wa kituo cha polisi. Katika kipindi hiki kumeanzishwa mradi wa ujenzi wa kituo cha polisi baada ya wananchi kuona umuhimu wa kuwepo na kituo hicho. Upo katika hatua za mwanzo

Tunashukuru idara ya maendeleo ya Jamii kuripatia vikundi 2 mikopo na hata kutupatia kabidhi boda boda siku ya Mwenge Wilaya

### TAARIFA ZA KISEKTA

I. **SEKTA YA ELIMU**-Shughuli za ufundishaji wanafunzi wa primary ( msingi) na sekondari uliendelea vizuri japo tatizo la uhaba wa walimu halijatatuliwa. Wanafunzi wa darasa la saba waliotarajiwa kufanya mitihani ya kumaliza walifanya mitihanihiyo kwa utulivu.

**II. SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO**

Kipindi hiki kilikuwa cha kuvuna . hali ya mavuno ni ya wastani kwani mazao yaliathiriwa na wadudu hatari aina ya “mbariti” yaani beanbellers na “ Nasheve” yaani cicadurina kwa upande wa maharage. Kwa upande wa mahindi mdudu aliyeshambulia ni maize stalkborer (kinyongo)

Wananchi walipatiwa mahindi na serikali ya kupunguza makali ya bei ya mahindi. Mahindi hayo yalikuwepo ya kutosha kadri ya mahitaji ya wananchi mahindi hayo yaliuzwa kwa bei ya sh. 800 kwa kilo

**SEKTA YA AFYA**

- Hakuna milipuko ya magonjwa iliyojitokeza
- Wagonjwa walihudumiwa kulingana na matatizo yaliyojitokeza
- Dawa zilikuwepo
- Wanachama waliojiunga na mfuko wa bima iliyoboreshwa ni 7 na kufanya jumla ya wanachama kuwa 17

**USAFI NA MAZINGIRA**

- Usafi wa jumla ulifanyika jumamosi ya mwisho wa mwezi
- Uharibifu wa mazingira uliojitokeza ni ule wa kuvuna mawe na mchanga sehemu zisizo kubalika. Hatua zilizochukuliwa ni kuwaonya wahusika na kutozwa faini

**TAARIFA ZA VIJIJI – KILOMENI**

Wananchi wa kijiji cha Kilomeni wamerejea maombi yao ya kugawa kijiji hicho viwe vijiji viwili. Jambo hili waliliwakilisha katika halmashauri ya wilaya wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa uliopita kwa bahati mbaya wakawa wamechelewa. Kufuatia jambo hili kamati ya maendeleo ya kata (WDC) imejadili na kuona hoja hiyo ina nguvu hivyo taarifa zifikishwe mapema kwenye kamati ya maendeleo ya wilaya.

**CHANGAMOTO**

Kwa kipindi hiki wananchi wapatao watatu (3) walijinyonga kwa kamba na kufariki dunia bila kupatikana sababu za maamuzi yao hayo magumu.

**MAOMBI**

(a) Tunaomba halmashauri ya wilaya ~~iharakishe~~ iangalie uwezekano wa upatikanaji wa mabati ya kuezekea chumba cha maabara shule ya sekondari Maghare ili kunusuru jengo kubomolewa na mvua

(b) Tunaiomba H/M kuangalia uwezekano wa kutupalia watumishi, hasa Afisa ugani – Mifugo : Vijiji na Kata. Kwani aliyepo ni I Hata hiyo ni tatizo.

**MWISHO**

Tunawashukuru viongozi na wakuu wa idara wa halmashauri ya wilaya, waheshimiwa madiwani kutupatia ushirikiano mara tulipohitaji huduma kwao.

Naomba kuwasilisha

[signature]

MWENYEKITI

[signature]

AFISA MTENDAJI KATA YA KILOMENI, MWANGA

KATIBU

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAY HADI SEPTEMBER 2017**

**UTANGULIZI**

1. Kata ya Toloha ipo katika Tarafa ya Jipe Ndea na ina Vijiji vitatu navyo ni Simu Kizungo, Gongoni na Karamba Ndea. Na ina Vitongoji 6 navyo ni Simu, Kizungo, Gongoni (A) Gongoni (B) Karamba na Ndea.

**I. MIPAKA**

Kwa upande wa Mashariki Kata imepakana na Nchi ya Kenya Magharibi imepakana na Kata ya Kwakoa Kaskazini imepakana na Kata ya Kigonigoni Kusini Magharibi imepakana na Kata ya Mgagao.

MIRADI YA KISECTA

**III. ELIMU**

Kata ya Toloha ina Shule za Msingi 2 nazo ni Shule ya Msingi Toloha na Shule ya Msingi Ndea. Shule ya Msingi ya Toloha ina upungufu wa madarasa mawili ambayo Wananchi wanaendelea mikakati na ujenzi wa madarasa hayo. Pia yupo Mfadhili ameahidi kuwapa nguvu Wananchi katika ujenzi wa madarasa hayo.

**UFAULU**

Wanafunzi waliomaliza darasa la saba katika Shule ya Toloha ni 33 waliofaulu ni 30 waliofeli ni 3. Katika Shule ya Karamba Ndea wanafunzi waliomaliza darasa la saba ni 17 waliofaulu ni 13 waliofeli ni 4. Choo cha Shule ya Msingi Toloha kimetitia, Kamati ya Shule na Wananchi wamekaa vikao na kuweka mikakati ya kuchimba shimo lingine .

**IV. AFYA**

Kata ya Toloha ina Zahanati 2 nazo ni Zahanati ya Toloha na Zahanati ya Karamba Ndea Wananchi waliojiunga na mfuko wa ICHF ni 12 .

**V. NJIA KUU ZA UCHUMI ZA WANANCHI KATIKA KATA**

Njia kuu za uchumi za Wananchi niufugaji na kilimo. Kwa kipindi hiki cha Vuli wananchi wanaendelea kuandaa mashamba , pia wamehamasishwa kuotesha mbegu ya muda mfupi

**ULINZI NA USALAMA KATIKA KATA YA TOLOHA.**

Ulinzi na usalama katika Kata ya Toloha ni shwari. Kwani hakuna tukio baya lililoripotiwa kwangu .

**VI. UHAMIAJI HARAMU**

Kwa kipindi cha miezi mitatu hakuna tukio lililoripotiwa la wahamiaji haramu.

**MAZINGIRA**

Kata ya Toloha uharibifu wa mazingira unaendelea kupungua – Kamati ya mazingira ya Kata na Kamati ya mazingira ya Vijiji wakishirikiana na Wananchi wema wanaendelea kupambana na

uharibifu wa mazingira huo. Pia nguvu ya kuzibiti uharibifu wa mazingira umeongezeka baada ya kupata vijana waliopata mafunzo ya ulinzi shirikishi kwa ajili ya Mali Asili.

**MAJI**

Kata ya Toloha ina miradi ya maji miwili

(a) Mradi wa Jua mato na mradi wa Karamba Ndea yote inaendelea kutoa huduma kwa Wananachi. Jumuiya ya Jua mato wameanza kupata huduma kwa kulipia huduma ya maji ambayo ni kila Kaya kwa mwezi ni Tshs ni Tshs 1,000/=. Na kwa sasa zimekusanywa Tshs 641,300/= kwa kipindi cha miezi mitatu.

**MAWASILIANO.**

Kata ya Toloha ina barabara kuu mbili

1. Barabara ya Kwakoa Toloha
2. Barabara ya Toloha, Karamba na Mgagao. Barabara zote mbili hazipitiki kwa urahisi kwani zinahitaji matengenezo.

Barabara ya Kwakoa Toloha inahitaji matengenezo kuwekwa makalvati kwani makalvati nane yamebomoka na mengine sita yameziba, pia kumwagwa vifusi maeneo korofi.

Barabara ya Toloha hadi Karamba kuna drafti ambayo imesombwa na maji na kusababisha magari kushindwa kupita kwa urahisi, kwa hiyo inahitaji matengenezo. Kutoka Karamba hadi Pangaro barabara ni mbovu sana kwani imekatika makorongo kiasi kwamba hata usafiri wa pikipiki inapitika kwa shida. Kwa hiyo inahitaji matengenezo makubwa tunaiomba Serikali kupitia barabara hiyo na kuona hali halisi ilivyo.

**VIKAO VYA KISHERIA NGAZI YA KATA NA VIJIJI**

| KATA | LENGO | HALISIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| TOLOHA | 1 | - | KUTOKUWA NA WENY VITI WA VIJIJI. |

**VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA KIJIJI**

| KATA | KIJIJI | VIKAO | HALISIA | MKUTANO MKUU | HALISIA |
|---|---|---|---|---|---|
| TOLOHA | KARAMBA NDEA | 3 | 1 | 1 | - |
| | SIMU KIZUNGO | 3 | 2 | 1 | 1 |
| | GONGONI | 3 | 1 | 1 | - |

**VIKAO VYA VITONGOJI**

| KATA | KITONGOJI | VIKAO | HALISIA |
|---|---|---|---|
| TOLOHA | SIMU | 3 | 2 |
| | KIZUNGO | 3 | 2 |
| | GONGONI A | 3 | 2 |
| | GONGONI B | 3 | 2 |
| | KARAMBA | 3 | 2 |
| | NDEA | 3 | 2 |

Kwa kipindi cha robo ya ~~tatu~~ KWANZA Vijiji vya Kata ya Toloha vilikusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kama inavyoonekana hapa chini.

| KIJIJI | LENGO | HALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| SIMU KIZUNGO | TSHS 150,000/= | - | - |
| KARAMBA NDEA | " 250,000/= | TSHS 100,000/= | - |
| GONGONI | " 150,000/= | - | - |

Mapato ya Halmashauri ya Vijiji vya Kata ya Toloha yalikusanywa kama ifuatavyo:-

| KIJIJI | LENGO | HALISIA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| SIMU KIZUNGO | TSHS 300,000/= | TSHS 470,000/= | - |
| GONGONI | " 200,000/= | " 100,000/= | - |
| KARAMBA NDEA | " 150,000/= | 2,00.2,500/= | - |

**CHANGA MOTO**

Baadhi ya Wananchi wamilimani Usangi walihamisha maji kutoka kwenye mto unaoingiza maji kwenye Intak ya Kata ya Toloha na kusababisha Wananchi wa Kata ya Toloha kukosa maji kwa muda wa miezi miwili.

**UTATUZI**

Mafundi bomba na Uongozi wa Kata ya Toloha walifuatilia maji hadi Usangi na kuwakuta watu wawili wamehamisha maji na kuelekeza kwenye mashamba yao. Watu hao walikamatwa na kufikishwa kituo cha Polisi Ngulu

**MWISHO**

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

------------------------------

**UMETHIBITISHWA LEO NA MH.DIWANI**
**KATA YA TOLOHA KINGA AMIRI LEO**
**TAREHE 14/11/2017**

AMTENDAJI KATA
TOLOHA

------------------------------

**TAARIFA HII IMEANDALIWA NA**
**NDG. M. MGANGA**
**AFISA MTENDAJI KATA YA TOLOHA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA KATA YA CHOMVU**

**KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2017**

**1. UTANGULIZI**

Kata ya Chomvu ipo Tarafa ya Usangi wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Kata hii imeundwa na vijiji vine(4) vyenye vitongoji 21. Vijiji hivyo ni Mshewa, Ndorwe, Kimbale na Chomvu.

Kata hii ina shule tano za msingi na shule nne za Sekondari.

Shule za Msingi ni, Ndorwe, Makandeni, Chomvu, Karambacha na Usangi.

Shule za secondari ni Ndorwe, Lomwe, Usangi Girls na Kirongaya.

**2. ULINZI NA USALAMA**

Hali ya ulinzi na usalama kwa kipindi hiki niya kuridhisha, matukio madogo madogo yaliyojitokeza yaliripotiwa vituo vya polisi vya Msangeni na Mwanga.

(i) **Migogoro ya wakulima na wafugaji** – hakuna

(ii) **Wahamiaji haramu** – Hakuna

(iii) **Migogoro ya Ardhi –** Mashauri 3 yamepokelewa baraza la Ardhi la Kata.

**3. VIKAO VYA KISHERIA**

**(a) Ngazi ya vitongoji**

Vimefanyika vikao 37 kati ya 63 vilivyokuwa vinahitajika vifanyike.

**(b) Ngazi ya Vijiji**

i. Vikaovya halmashauri ya kijiji – vikao 12 vimefanyika kati 12 vilivyokuwa vinatakiwa

ii. Mikutano mikuu ya vijiji – mikutano minne (4) imefanyika kati ya mnne (4) iliyokuwa inatakiwa

**(c) Ngazi ya kata**

Kimefanyika kikao kimoja cha W.D.C kati ya kimoja kilichokua kinatakiwa kifanyike.

**4. HALI YA CHAKULA**

Hali ya Chakula kwa sasa niya wastani.

**5. UKUSANYAJI WA MAPATO**

Jumla ya Tshs 123,000/= kimekusanya ambazo ni ada ya leseni za biashara na vileo.

**6. UHARIBIFU WA MAZINGIRA**

Limeripotiwa tukio la moto uliokua unaelekea katika msitu wa asili wa Kena kijiji cha Mshewa. Wananchi walijitokeza kwa wingi na kuuzima moto huo kabla haujafika kwenye msitu.

**7. MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA**

**(a) UJENZI WA OFISI YA KATA CHOMVU**

Kazi ya ujenzi wa ofisi ya Kata inaendele, hatua iliyofikia kwa sasa jengo linapigwa bati.

**(b) AFYA**

i. **iCHF,** wananchi wanaendelea kuelimishwa kujiunga na mfuko wa **iCHF**, ila mwiitiko ni mdogo sana. Kwa kipindi hiki waliojiunga ni kama ifuatavyo:-

- Kijiji cha Ndorwe Kaya 15 Tshs 450,000/=
- Kijiji cha Mshewa Kaya 26 Tshs 780,000/= **JUMLA NI TSHS 1,710,000/=**
- Kijiji cha Chomvu Kaya 16 Tshs 480,000/=

ii. **Malipo la papo kwa papo**, zimepokelewa Tshs 28,000/= zahanati ya Ndorwe.

iii. **Ujenzi wa zahanati Vyanyua** – Ujenzi wa kuta umefikia kufunga lenta. Hitaji kubwa lililopo mbele yetu ni nondo na saruji kwa ajili ya kuweka lenta. Kazi hii ya kuweka lenta inahitajika mapewa kabla ya mvua za vuli hazijachanganya kwani zinaweza kusababisha uharibifu wa kuta.

Tayari tumesha mwandikia mkurugenzi mtendaji wilaya kuomba saruji na nondo.

**(c) BARABARA**

Wananchi wanaendelea kukarabati barabara ili ziendelee kutumika.

**(d) ELIMU**

**i. Taaluma**

Jumla ya wanafunzi 178 (WAV- 83, WAS- 95) wa darasa la saba wamefanya mitihani yao ya utimilifu elimu ya msingi 2017

ii. **Ujenzi wa vyumba vya madarasa S/M Chomvu,** ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa S/M Chomvu unaendelea na jengo limepauliwa.

**(e) KILIMO**

Shughuli za kilimo zinaendelea kwa sasa ni kuandaa mashamba kwaajili ya msimu wa vuli 2017/2018

**CHANGAMOTO**

Changamoto kubwa ni kuhusu vifaa vya kuwekea lenta zahanati ya Vanyua, kwani tunahofu ikinyesha mvua kubwa inaweza kuangusha kuta.

**UTATUZI**

Tayari ameshaandikiwa mkurugenzi mtendaji (w) ombi la kutoa nondo na saruji tunahitaji mrejesho wa haraka.

**Mh. Mwenyekiti naomba kuwasilisha**

.............................................. ..............................................

**Mh. Eliasikia S. Mchomvu** **Bw. Omari S. Kiangi**

**Diwani Kata ya Chomvu** **Afisa Mtendaji Kata**

**Tarehe 03/11/2017**

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATA KWAKOA JULAY – SEPTEMBER 2017.

## UTANGULIZI:-

Kata ya Kwakoa ni mojawapo ya kata tano zinazounda Tarafa ya Jipe Ndea.

Kata hii ina vijiji viwili, vitongoji saba, wakazi wake ni wakulima na wafugaji wapatao 3717 kwa mujibu wa sensa ya 2012.

Kata hii ina Madarasa ya awali Matatu, Shule za Msingi Tatu na Sekondari Moja ya Serikali pia zipo Zahanati Mbili moja ya Serikali na ya pili inamilikiwa na Jimbo Katoliki Same.

## ULINZI NA USALAMA.

Hali ya Ulinzi na Usalama ni nzuri kiasi.

1. Yapo Matukio yaliyojitokeza hasa kwa kipindi chote cha Julay – September 2017. Makundi makubwa ya Tembo toka hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Hifadhi ya Tsavo nchini Kenya yalivamia mashamba ya wakulima wapatao Mia Moja na Moja (101) na kuharibu aina zote za mazao yaliyokuwa shambani kama vile Matikiti, Nyanya, Migomba, Miwa, Nazi, Miembe na Parachichi.
   Wakulima hao wametakiwa kujaza fomu za kuomba kifuta jasho kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii.
2. Kumekuwa na kugawanyika kwa Serikali ya kijiji cha Kwakoa, suala ambalo limekwamisha kuendelea kwa miradi ya maendeleo kijijini na kuendeleza migogoro mbali mbali ndani na nje ya kijiji.

## VIKAO VYA KISHERIA.

(1) WDC Lengo 1 Halisi 1

(2) Vikao vya Halmashauri za Vijiji

| | Lengo | Halisi | Mengineyo |
|---|---|---|---|
| Ngulu | 3 | 2 | Bado 1 |
| Kwakoa | 3 | 3 | - |

Mikutano ya Hadhara kwa ajili ya kusoma Mapato na Matumizi

| | Lengo | Halisi |
|---|---|---|
| Ngulu | 1 | 1 |
| Kwakoa | 1 | bado |

Mikutano ya Vitongoji

| | Lengo | Halisi | Mengineyo | |
|---|---|---|---|---|
| Ngulu | 12 | 4 | bado | 8 |
| Kwakoa | 9 | 5 | bado | 4 |

Taarifa za Kisekta.

Bima ya Afya iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti waliojiunga na Bima ya Afya ni,

Ngulu - 18

Kwakoa - 5

MAJI.

Mheshimiwa Mwenyekiti tunashukuru Serikali na Halmashauri ya Wilaya kwa ukarabati wa Chanzo cha Maji Ngongo na Kisingari kijiji cha Ngulu, pia birika la kunyweshea Mifugo kwa thamani ya shilingi 37,114,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti tunaendelea kukushukuru na Serikali yetu kwa ujenzi wa mradi wa maji Kwakoa hasa ujenzi wa Tanki, Birika la kunyweshea mifugo, Ujenzi waVituo vya Jamii 17 na ukarabati wa miundo mbinu mradi wa zamani kwa shilingi 199,840,289/=

Mradi umekamilika kwa asilimia 98%

ELIMU.

Upauaji wa vyumba viwili vya madarasaShule ya Msingi Ngulu.

Kazi iliyofanyika ni Ununuzi wa Mbao za kupaulia 2,900,000/= [→ 290] zenye thamani ya shilingi 1,175,000/= Tunaomba H/mashauri isaidie kumalizia vyumba viwili vilivyo baki.

Hakuna mradi mwingine unaendelea kwa kipindi hiki.

Ukusanyaji wa Mapato

Kwakoa 595,000/=

Ngulu Hakuna.

CHANGAMOTO.

(a) Uvamizi wa Tembo katika maeneo ya makazi na mashamba
(b) Migongano ya baadhi ya wajumbe wa Serikali ya Kijiji..

UTATUZI.

Idara ya wanyama pori wameshirikishwa.

Migogoro ya wajumbe wa Halmashauri za Vijiji.

Vikao vimeitishwa na vinaendelea kuitishwa ili kumaliza tofauti zinazojitokeza kati yao na Mwenyekiti wa Kijiji.

Naomba kuwasilisha

Saini ya Mwenyekiti.

Saini ya Katibu.

1. **SEHEMU YA KWANZA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA MAENDELEO YA KATA YA MGAGAO KUANZIA KINDI CHA MWEZI WA JULAI HADI SEPTEMBA 2017 KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2017/2018**

2. **SEHEMU YA PILI**

i. Kata ya Mgagao inapakana na Wilaya ya Same kwa upande wa kusini,magharibi kirya,kaskazini lembeni na mashariki inapakana na kata ya kwakoa.

ii. **UTAWALA-**Kata ina vijiji vitatu ambavyo ni Pangaro,Kiverenge na Mgagao,kata inajumla ya vitongoji 13.

iii. **ELIMU-**Kata ya Mgagao ina jumla ya shule sita(6).
Mgagao sekondari na Shule za msingi ni Mgagao, Kamani, Kauzeni,Kingondi na Kiverenge .

iv. **AFYA-**Kata ya mgagao ina jumla ya zahanati 2,Zahanati ya mgagao na zahanati ya Pangaro.Pia kuna klinlik ya wanawake iliyoko kijiji cha Pangaro .

v. **Uchumi**-Shughuli kubwa ya wakazi wa kata hii ni ufugaji,kilimo na biashara.

3. **SEHEMU YA TATU**

Hali ya Ulinzi na usalama ni wakuridhisha.

4. **SEHEMU YA NNE**

I. **VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA**

| Na. | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MGAGAO | 1 | 1 | Dharura 1 |

II. **VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI VILIVYOFANYIKA NI KAMA IFUATAVYO:**

| Na. | KIJIJI | VIKAO | | MIKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| 1. | MGAGAO | 3 | 3 | 1 | 1 | Kikao 1 cha Dharura |
| 2. | KIVERENGE | 3 | 2 | 1 | 1 | |
| 3. | PANGARO | 3 | 3 | 1 | 1 | |

III. **MIKUTANO YA WAKAZI NGAZI YA VITONGOJI**

| Na. | KIJIJI | VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MGAGAO | 5 | 15 | 6 | - |
| 2. | KIVERENGE | 4 | 12 | 4 | - |
| 3. | PANGARO | 3 | 9 | 4 | - |

## 5. SEHEMU YA TANO

**MAPATO NA MATUMIZI**

**I. TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI ZILIZOSOMWA KWENYE MIKUTANO MIKUU YA VIJIJI,**

| Na | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MGAGAO | 1 | 1 | |
| 2. | KIVERENGE | 1 | 1 | |
| 3. | PANGARO | 1 | - | |

**II. MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YAKO KAMA IFUATAVYO;**

| Na | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MGAGAO | 916,600 | 161,000 | 17.6 | |
| 2. | KIVERENGE | 40,000 | - | 0 | |
| 3. | PANGARO | - | - | - | - |

**III. MAPATO YA HALMASHAURI ZA VIJIJI**

Mapato ya Halmashauri za vijiji yalikusanywa kama ifuatavyo:

| Na. | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MGAGAO | 176,000 | 427,200 | 242.7 | |
| 2. | KIVERENGE | 150,000 | 600,000 | 400 | |
| 3. | PANGARO | - | 300,000 | | |
| | JUMLA Tsh. | 326,000 | 1,327,200 | | |

## 6. SEHEMU YA SITA

MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA

I. MIRADI YA MAENDELEO

**SEKTA YA ELIMU**

| JINA LA MRADI | LENGO LA MRADI | UTEKELEZAJI | RUZUKU TOKA SERIKALI KUU | FEDHA TOKA SEHEMU NYINGINE | NGUVU KAZI YA WANANCHI | GHARAMA ZA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba 2 vya maabara | Kujenga vyumba 2 vya maabara | Michango inaendelea kukusanywa | - | - | | 162,000,000/= |
| Ujenzi wa choo katika shule ya msingi Kingondi | Kujenga choo | Ujenzi umefikia hatua ya bado sakafu sehemu ya mbele ya choo na milango | | Fedha toka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ni Tsh.3,500,000 | Kuchimba shimo la choo na mawe roli 6 na mchanga roli 1 | 3,500,000 lakini bado fedha za milango hazikujumuishwa katika bajeti hiyo. |

**SEKTA YA MIFUGO**

| NA LA MRADI | LENGO LA MRADI | UTEKELEZAJI | RUZUKU TOKA SERIKALI KUU | FEDHA TOKA SEHEMU NYINGINE | NGUVU KAZI YA WANANCHI | GHARAMA ZA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa mnada wa mifugo mgagao katika eneo ya zizi la mifugo. | Kukarabati eneo la zizi la Ng'ombe Mgagao. | Ukarabati bado haujaanza. | - | | - | Tsh.24,708,000/= |
| Ujenzi wa uzio wa mnada wa mifugo | Kujenga uzio kuzuia mifugo isitoroshwe wakati wa mnada. | Sehemu ya ukarabati wa uzio imekamilika | - | Fedha kutoka ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji 2,705,000/= | - | |

II. TAARIFA ZA KISEKTA (IDARA ZINAZOTOA HUDUMA)

**Kilimo-**Ushauri kwa wakulima kuhusu kilimo bora unatolewa.

**Mifugo-**Huduma za ugani zilizotolewa ni tiba,chanjo na ushauri kwa baadhi ya wafugaji.Tunaishukuru ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wilaya kwa kutujengea uzio wa mifugo katika mnada wa mifugo hali inayosaidia kuzuia utoroshaji wa mifugo na kuzuia upotevu wa mapato ya Halmashauri.

**Afya-**Huduma zilizotolewa kwa kipindi hicho ni pamoja na tiba,chanjo na ushauri wa kitabibu.

**Elimu-**Hali ya elimu katika kata ni ya kuridhisha,

**Maendeleo ya jamii-** Idara imetoa mafunzo ya ujasiliamali kwa vikundi vya vikoba na baadhi ya vikundi vimeomba mikopo hasa vya wanawake kutoka mfuko wa wanawake na vijana.

7. **SEHEMU YA SABA**

I. **CHANGAMOTO**

1. Baadhi ya Askari polisi kufanya doria isiyo rasmi na kuwanyanyasa wananchi kwa kuwatoza fedha kama fain na kutowapatia risiti hasa siku za ijumaa,hivyo kuchangia kungezeka kwa vitendo vya uhalifu.
2. Ukosefu wa usafiri kwa watumishi na wataalam hivyo kuchangia baadhi ya maeneo kutokufikika kwa wakati.
3. Ubovu wa barabara ya kutoka Mgagao kuelekea Pangaro kwa sasa inapitika kwa shida.

**II. MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO HIZO**

- Sheria,kanuni na taratibu zitumike kupunguza au kutatua migogoro na changamoto mbalimbali.

8. **SEHEMU YA NANE**

MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

**I. MAPENDEKEZO**

1. Ni vyema askari polisi wanaofika kwa ajili ya doria watoe taarifa kuhusiana na watuhumiwa waliowakamata na makosa yao.
2. Halmashauri ya Wilaya ifanye mpango wa kukarabati kwa Haraka katika barabara ya Mgagao-Pangaro hadi Toroha ili kuondoa adha kwa watumiaji wa barabara hiyo.
3. Halmashauri ya Wilaya ijenge zizi la mifugo katika mnada wa Mgagao kwani wateja wanalalamika kutokana na upotevu wa mifugo unaotokea mara kwa mara.
4. Halmashauri ya Wilaya ikarabati malambo ya maji ya kauzeni na Doya ili kusaidia wafugaji walioko maeneo hayo.

**II. HITIMISHO**

NAOMBA KUWASILISHA,

TAARIFA HII IMEDHIBITISHWA LEO NA

| | |
|---|---|
| [MH. DIWANI KATA YA MGAGAO] | [MTENDAJI KATA YA MGAGAO] |
| LONGOVIRO ARPAKWA KIPUYO] | MAGESA KEYA |
| ……………… | …………………………… |
| TAREHE 14/11/2017 | TAREHE 14-11-2017 |

AFISA MTENDAJI KATA YA MGAGAO

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI NA SHUGHULI MBALIMBALI YA ROBOYA KWANZA JULAI-SEPTEMBA 2017 KATA YA LEMBENI KWA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA TAREHE 04 NOVEMBA 2017.**

## 1.SEHEMU YA KWANZA.

### I .0 UTANGULIZI

### 1.0.1 ENEO LA MIPAKA.

Kata ya Lembeni inapakana na Kata ya Ngujini na Kilomeni kwa upande wa Mashariki, Kata ya Mgagao upande wa Kusini Kata ya Kirya na Lang'ata upande wa Magharibi na mamlaka ya mji mdogo Mwanga kwa Upande wa Kaskazini.

### 1.0.2 UTAWALA

Kata ina jumla ya vijiji vitano (5) na vitongoji 25 na idadi ya wakazi ME 11,780 na KE 6,114 kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012.

### 1.0.3 HALI YA WATUMISHI KWENYE KATA

| NO. | IDARA | AINA YA WATUMISHI | MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | UTAWALA | MTENDAJI WA KATA | 1 | 1 | - |
| | | WATENDAJI WA VIJIJI | 5 | 2 | 3 |
| 2. | ELIMU | MRATIBU ELIMU KATA | 1 | 1 | - |
| | | WALIMU SHULE YA MSINGI | 80 | 63 | 17 |
| | | WALIMU SEKONDARI | 89 | 77 | 12 |
| | | CHUO CHA USTAWI | | 26 | |
| 3. | MIFUGO | AFISA MIFUGO KATA | 1 | 1 | - |
| | | AFISA MIFUGO VIJIJI | 5 | 3 | 2 |
| 4. | KILIMO | AFISA KILIMO KATA | 1 | 1 | - |
| | | AFISA KILIMO KATIKA VIJIJI | 5 | 4 | 1 |
| 5. | AFYA | AFISA AFYA | 1 | 1 | - |
| 6 | MAENDELEO YA JAMII NA USTAWI WA JAMII. | AFISA MAENDELEO YA JAMII NA AFISA USTAWI WA JAMII | 2 | - | 2 |

### 1.0.4 ELIMU

Shule za Msingi

Kata ina jumla ya shule za msingi 9 ambazo ni shule ya msingi Kiruru, shule ya msingi Kisangara, shule ya msingi Chanjale, shule ya msingi Mangara, shule ya msingi Msafiri Medium(binafsi) , shule ya msingi Mbambua, Shule ya Msingi Kaili, shule ya Msingi Lembeni, na shule ya Msingi Kisekibaha.

**Shule za Sekondari**

Zipo shule za sekondari tano (5) Shule za Serikali ni mbili(2) ambazo Nyerere Sekondari ,Kisangara Sekondari, Shule za Binafsi ni tatu(3) Chanjale Seminary Sekondary, St,Stephen Sekondari na One World Sekondari.

**Vyuo**

Chuo cha Serikali ni kimoja( 1) ambacho ni chuo cha Ustawi wa Jamii na vyuo 2 vya ufundi ambavyo ni chuo cha Ngwalu na Malage (binafsi).

**IDADI YA WALIMU.**

Idadi ya Walimu

Shule za Msingi Jumla ni 63

Shule za Sekondari Jumla ni 77.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA ELIMU BILA MALIPO

Kipindi cha Julai-Septemba 2017 shule za Msingi zilipokea Jumla ya Tsh.8,689,213.1 na matumizi 7,655,630.00 baki Tsh.1,033,583.1 ambazo zipo benki , na shule za Sekondari zilipokea Tsh.42,564,117.00 , Jumla ya Tsh.31,440,980.14 zimetumika na zilizobaki benki ni Tsh.11,123,136.86.

## TAALUMA

Masomo yote yanafundishwa kwa kufuata ratiba kuu ya shule kutokana na mtaala mpya na wa zamani .Utoaji wa taaluma ni mzuri kwa shule za msingi na Sekondari.

Wanafunzi wa darasa la saba 2017 waliofanya mtihani jumla ni 317 Wav 153 , Was164.

### 1.0.5 AFYA

Kata ina vituo vya huduma za Afya 2 vituo ni Zahanati ya Kiruru na Kituo cha Afya Kisangara.

### 1.0.6 SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Shughuli za kiuchumi kwa wakazi wa Kata ya Lembeni ni Kilimo, Ufugaji na Biashara ndogondogo.

## 2. SEHEMU YA PILI

### 2.0 ULINZI NA USALAMA.

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Kata ya Lembeni kwa kipindi cha Julai-Septemba 2017 kwa ujumla ni ya kuridhisha.

## 3. SEHEMU YA TATU

### 3. 0 VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA;

Vikao na mikutano ya kisheria ngazi ya Kata, vijiji na vitongoji imefanyika kama ifuatavyo katika kipindi hiki cha robo ya kwanza ya mwaka 2017;

### 3.0.1 VIKAO VYA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA (WDC)

| Na. | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | LEMBENI | 1 | 1 | - |

### 3.0.2 VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI

| KATA | VIJIJI | VIKAO (H/KIJIJI) | | MIKUTANO MIKUU | |
|---|---|---|---|---|---|
| LEMBENI | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI |
| | KIRURU IBWEJEWA | 3 | 3 | 1 | 1 |
| | KISANGARA | 3 | 2 | 1 | 1 |
| | MANGARA | 3 | 3 | 1 | 1 |
| | MBAMBUA | 3 | 2 | 1 | 1 |
| | LEMBENI | 3 | 2 | 1 | 1 |

### 3.0.3 MIKUTANO YA WAKAZI WA VITONGOJI;-

| KATA | VIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| LEMBENI | KIRURU IBWEJEWA | 4 | 12 | 6 | |
| | KISANGARA | 10 | 30 | 10 | |
| | MANGARA | 3 | 9 | 6 | |
| | MBAMBUA | 4 | 12 | 8 | |
| | LEMBENI | 4 | 12 | 4 | |

## 4. SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAPATO NA MATUMIZI

Ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na vijiji katika Kata ya Lembeni ilikuwa kama ifuatavyo;

#### 4.0.1 MAPATO YA H/WILAYA

Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2017 vijiji vya Kata ya Lembeni vilikusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya jumla ya Tsh. 667,000.00 na mchanganuo wa mapato haya umebainishwa kwenye jedwali lifuatalo ;

| KATA | VIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| LEMBENI | KIRURU IBWEJEWA | 210,000.00 | 100,000.00 | 48% | |
| | KISANGARA | 389,250.00 | 247,000.00 | 63% | |
| | MANGARA | 185,500.00 | 63,000.00 | 34% | |
| | MBAMBUA | 52,000.00 | - | 0% | |
| | LEMBENI | 257,000.00 | 257,000.00 | 100% | |
| | | | | | |
| JUMLA | | 1,093,750.00 | 667,000.00 | 61% | |

#### 4.0.2 MAPATO YA HALMASHAURI ZA VIJIJI KATA- LEMBENI.

Mapato ya Halmashauri za vijiji Kata ya Lembeni yalikusanywa kama ifuatavyo;-

| KATA | VIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| LEMBENI | KIRURU IBWEJEWA | 575,000.00 | 315,000.00 | 55% | |
| | KISANGARA | 267,500.00 | 175,000.00 | 65% | |
| | MANGARA | 75,000.00 | 52,500.00 | 70% | |
| | MBAMBUA | 510,000.00 | 340,000.00 | 67% | |
| | LEMBENI | 500,000.00 | 565,000.00 | 113% | |
| | JUMLA | 1,927,500.00 | 1,447,500.00 | 75% | |

## 5. SEHEMU YA TANO

### 5.0 MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI;

#### 5.0.1 ELIMU

| JINA LA MRADI | LENGO LA MRADI | UTEKELEZAJI | RUZUKU TOKA SERIKALI KUU | FEDHA TOKA HALMASHAURI | MICHANGO YA WANANCHI | GHARAMA ZA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa choo cha wanafunzi matundu 16 S/Msingi Chanjale | Ukamilishaji ujenzi wa choo matundu 16 | Ujenzi umefikia usawa wa mita mbili | - | - | 162,000.00 | 9,769,730.00 |
| Ujenzi wa choo matundu 4 S/Msingi Kaili | Ukamilishaji ujenzi wa choo matundu 4 | Hakuna | - | - | Mifuko 5 ya Saruji | 5,800,000.00 |
| Kukamilisha Ujenzi wa Darasa,Ofisi ya Mwalimu na Stoo S/Msingi Kisekibaha | Kukamilisha ujenzi wa viporo vya ujenzi huo. | Hakuna | - | - | - | 6,000,000.00 |
| Ujenzi wa Bweni la wavulana katika | Kukamilisha ujenzi wa Bweni. | Jengo limeezekwa kupiga lipu,niru,sakafu | - | 15,000,000.00 | - | 25,000,000.00 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sekondari ya Nyerere | | ,milango na madirisha,kujenga ngazi tatu jumla zimetumika Tsh.14,000,000.00 Zinahitajika Tsh.500,000.00 kwa ajili ya kuweka umeme. | | | | |
| Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika S/Msingi Mbabua | Ukamilishaji wa vyumba 3 vya madarasa | Ujenzi bado haujaanza | - | - | Kwa kipindi hiki wananchi wamekusanya Roli 20 za mawe. | 24,581,000.00 |

**ii) AFYA**

| JINA LA MRADI | LENGO LA MRADI | UETEKELEZAJI | RUZUKU TOKA SERIKALI KUU | FEDHA TOKA HALMASHAURI YA WILAYA | MICHANGO YA WANANCHI | GHARAMAZA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa choo na shimo la choo katika nyumba ya Mganga Zahanati ya Kiruru. | Kukamilisha ujenzi wa choo . | Ujenzi umekamilika fedha zilizotumika ni Tsh.1,754,000.00, Na Tsh.246,000.00 zimebaki. | | 2,000,000.00 | | 2,000,000.00 |

**iii) UTAWALA**

| JINA LA MRADI | LENGO LA MRADI | UTEKELEZAJI | FEDHA TOKA KWA MKURUGENZI | FEDHA TOKA SERIKALI KUU | MICHANGO YA WANANCHI | FEDHA TOKA KWA WAFADHILI | GHARAMA HALISI ZA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa choo matundu 4 kukamilisha na kukarabati ujenzi wa kituo cha polisi Kisangara | Ukamilishaji wa kituo cha polisi na ujenzi wa choo matundu 4. | Ujenzi umekamilika na umeme tayari umekwishaingia. | | - | 5,752,400.00 | - | 5,752,400.00 |

## 6. SEHEMU YA SITA

## 6.0 TAARIFA ZA IDARA MBALIMBALI

### 6.0.1Elimu

Hali ya utoaji wa taaluma ni nzuri kwa shule za Msingi na Sekondari. Shirika la World Vision linatoa mchango wa Elimu kwa kutumia wataalam wake kufundisha wanafunzi wa darasa la 1hadi la 3 kwa kuwaongezea uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu kwa siku za kila jumamosi kuanzia saa tatu kamili asubuhi hadi saa saba kamili mchana.

### 6.0.2 Afya

Mfuko wa Bima ya Afya;

ananchi ya Kata ya Lembeni walihimizwa kujiunga na mfuko wa wa Bima ya Afya ulioboreshwa Ichf kama ifuatavyo;-
Hali ya uchangiaji wa mfuko huu badounasua katika vijiji vyote vya kata ya Lembeni . Sera ya Wizara ya Afya ni kuhakikisha kuwa kila kaya inajiunga na mfuko wa Bima ya Afya .
Mpaka sasa hivi hali iko kama inavyobainishwa kwenye jedwali hapa chini;

**IDADI YA KAYA ZILIZOJIUNGA NA iCHF KWA ROBO YA KWANZA JULY-SEPTEMBA 2017.**

| JINA LA KIJIJI | LENGO KWA MWAKA | LENGO LA ROBO MWAKA | HALI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| KISANGARA | 440 | 110 | 5 | 4.5 |
| MBAMBUA | 96 | 24 | 1 | 4.2 |
| LEMBENI | 244 | 61 | 3 | 4.9 |
| MANGARA | 180 | 45 | 5 | 11.1 |
| KIRURU | 172 | 43 | 9 | 20.9 |
| JUMLA | 1,132 | 283 | 23 | 8.1 |

**Usafi wa Mazingira**

Jumla ya kaya 2,247 na kuonyesha kuwa 96.4% ya kaya zote walikuwa na choo ,na 3.5% hawana choo kabisa. 83.6% ya kaya zote zina vyoo bora.
Suala la utupaji taka bado nichangamoto kubwa katika kata yetu. 50% t undo wana mashimo ya taka na sehemu iliyobaki taka hutupwa ovyo na kusababisha kuzagaa kwa taka kila kona hususani maeneo ya wazi na kandokando ya barabara. Jitihada za kuhamasisha jamii zinaendelea kufanyika katika shughuli zetu za kila siku na kila jumamosi ya mwiho wa mwezi.

**<u>Vyanzo Vya Maji;</u>**

Vyanzo vyetu vya maji bado ni salama ingawa maji yake si salama.
Kwa kipindi chote cha robo ya kwanza ya mwkw 2017 (Julai-Septemba) kata hii haikukumbwa na magonjwa ya mlipuko .Hata hivyo wagonjwa 4 walilipotiwa katika kituo cha Afya Kisangara kwa kung'atwa na Mbwa na walipatiwa huduma wanaendelea vyema

**6.0.3 MIFUGO**

**USHAURI ULIOTOLEWA;**

Kwa kipindi hiki ushauri ulitolewa kwa wafugaji kama ifuatavyo;

| MWEZI | ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|---|
| JULAI | 42 | 66 | 108 |
| AGOSTI | 79 | 29 | 108 |
| SEPTEMBA | 58 | 86 | 144 |
| JUMLA | 179 | 181 | 360 |

**<u>MAGONJWA YA MLIPUKO KWA MIFUGO;</u>**

Hakuna magonjwa ya Mifugo yaliyolitokea ispokuwa magonjwa ya kawaida kama inavyoonyesha hapa chini kwenye jedwali la matibabu kwa Mifugo.

**<u>MATIBABU KWA MIFUGO;</u>**

| WANYAMA | UGONJWA | PATWA | TIBIWA | PONA | KUFA | DAWA ILIYOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ng,ombe | Ndigana kali | 9 | 9 | 8 | 1 | Paruaquone inj. Otc 20% inj |
| Ng,ombe | Ndigana aridi | 76 | 76 | 74 | 2 | OTC Inj.+Liquid P. |
| Ng,ombe | Minyoo | 246 | 246 | 246 | - | Albendazole |
| Mbuzi | Minyoo | 484 | 484 | 480 | 4 | Albendazole |
| Kondoo | Minyoo | 316 | 316 | 316 | - | Albendazole |

Magonjwa yaletwayo na Virus na chanjo imetolewa;-
a)Kideri (mdondo)-Kuku 4600
b)Ndui ya kuku-Kuku 1450
c)Gumboro-Kuku 360

**MALENGO YA ADA YA UKAGUZI WA NYAMA KATA YA LEMBENI 2017/2018**

| KIJIJI | IDADI YA NG'OMBE | IDADI YA MBUZI | IDADI YA KONDOO | MALENGO YA ADA |
|---|---|---|---|---|
| KIRURU IBWEJEWA | 36 | 72 | 80 | 175,600.00 |
| KISANGARA | 480 | 140 | 302 | 1,091,600.00 |
| LEMBENI | 48 | - | - | 72,000.00 |
| JUMLA | 564 | 212 | 382 | 1,349,200.00 |

**MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA (ADA YA UKAGUZI WA NYAMA)**

Kwa kipindi hiki mapato ya ukaguzi wa nyama ilikuwa kama ifuatavyo;.

| NG'OMBE | MBUZI/KONDOO | JUMLA | JUMLA YA MAPATO YA H/WILAYA |
|---|---|---|---|
| 154 | 144 | 298 | 345,200.00 |

### 6.0.4 KILIMO;-

Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2017 shughuli za kilimo zilifanyika kuhamasisha wakulima kuandaa mashamba mapema kabla ya mvua za vuli kuanza, kuhamasisha wakulima kuweka mbolea ya samadi kwenye mashamba yao, kuwatembelea wakulima wa mbogamboga na matunda kuwashauri kilimo bora cha mboga,matumizi sahihi ya viuadudu kwenye mashamba yaliyo athirika na magonjwa.

**IDADI YA WAKULIMA WALIOTEMBELEWA NA KUPATIWA USHAURI**

Jumla ya wakulima 196 walitembelewa na kupatiwa ushauri mbalimbali kama inavyoonyesha kwa kila kijiji katika jedwali hili;-

| KIJIJI | KISANGARA | KIRURU | MANGARA | LEMBENI | MBAMBUA |
|---|---|---|---|---|---|
| IDADI YA WANAWAKE | 29 | 72 | 13 | 5 | 8 |
| IDADI YA WANAUME | 16 | 40 | 9 | 1 | 3 |
| JUMLA | 45 | 112 | 22 | 6 | 11 |

**MAGONJWA NA WADUDU WALIOATHIRI MBOGAMBOGA NA MATUNDA;**

| JINA LA UGONJWA | MIMEA ILIYOATHIRIKA | UKUBWA WA ENEO | DAWA ILIYOTUMIKA |
|---|---|---|---|
| Aphids | Mchicha, mnavu na maua | 0.4 h | Dudu all, Dudu baa |
| Powder Mildew | Mapapai na Machungwa | 0.4 h | Ridomil |
| Green Catapila | Kabeji | 0.5 | Spidex |
| Blight | Nyanya | 0.5 | Ridomil,Verytigo |

**MAVUNO YA MBOGAMBOGA**

Jumla ya viroba 455 vya mbogamboga vimevunwa.

**MAVUNO HALISI YA CHAKULA KATIKA KATA**

| ZAO | KIASI |
|---|---|
| MAHINDI | 557.4 tani |
| KUNDE | 87.5 tani |
| CHOROKO | 120 tani |
| MAHARAGE | 36.8 tani |
| MTAMA | 4.6 tani |
| VIAZI VITAMU | 2 tani |
| FIWI | 1.5 tani |
| MIHOGO | 4.5 tani |
| MBAAZI | 1.4 tani |
| KARANGA | 4.8 tani |

## 7. SEHEMU YA SABA

### 7.0.1 CHANGAMOTO

a)Kuna uchakavu wa vyumba vya Madarasa ya chekechea na elimu ya watu wazima
b) Kutokuwa na walimu wa kudumu wa madarasa ya chekechea na elimu ya watu wazima
c) Upungufu wa matundu ya vyoo vya wanafunzi katika shule zote zilizomo ndani ya kata
d) Uhaba wa maji kwenye vijiji vyote vya kata ya Lembeni
e) Upungufu wa walimu wa Sayansi na Hisabati
f)Wananchi kuvamia maeneo ya shule na ofisi za serikali za vijiji
g) Kuwepo kwa mbwa wanozulula na kushambulia mifugo na binadamu.

### 7.0.2 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

a)Kumuandikia Mkurugenzi pamoja na kufanya jitihada za kutafuta wafadhili mbalimbali wa kutusaidia katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na mabweni, ujenzi wa vyoo vya wanafunzi,ujenzi wa miundombinu ya maji.
b)Kushirikiana na uongozi wa kijiji kuhimiza wananchi kuchangia michango mbalimbali ya miradi ya maendeleo kama sehemu ya majukumu yao.
c)Kushirikiana na wazazi wa Wanafunzi wanaosoma sayansi kuchangia fedha za kutafuta walimu wa masomo husika ili waweze kufundishwa somo ambalo halina Mwalimu.
d)Kumuandikia Mkurugenzi kuwaagiza Afisa ardhi kupima maeneo yote ya ofisi za serikali za vijiji na shule zote zilizomo ndani ya kata .
e)Kuhimiza wafugaji wa mbwa kufunga Mbwa wao na Mbwa ambao wana vichaa kuweka mikakati ya kuwaua.
Naomba kuwasilisha,
Taarifa hii imeandaliwa na

| | |
|---|---|
| ................................................ | ................................................ |
| **Godwin Vincent Mmbaga** | **Advella S.Ntangeki** |
| **Mh, Diwani, Kata ya Lembeni** | **Afisa Mtendaji, kata ya Lembeni** |
| | AFISA MTENDAJI<br>KATA YA LEMBENI |

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA KILEO KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA JULAI-SEPTEMBA 2017

### 1.0 .UTANGULIZI

Kata ya Kileo ni miongoni mwa kata ishirini(20) za wilaya ya Mwanga.Kata hii imepakana kwa upande wa Kaskazini na wilaya ya Moshi vijijini,Kusini Mamlaka ya mji mdogo Mwanga,Mashariki nchi ya Kenya na Magharibi Moshi vijijini.Kiutawala,kata ya Kileo ina vijiji vine(4) ambavyo ni Kifaru,Kileo, Kituri na Kivulini;aidha kuna jumla ya vitongoji kumi na saba(17).Kwa upande wa elimu,kata hii ina shule za Msingi kumi na moja ambazo ni Kifaru,Majengo,Kitopeni,Kituri,Kalimani,Mnoa,Kileo,Mkombozi,Kivulini,Muungano na Testimony English Medium School ambayo ni ya binafsi.Shule za Sekondari ni tatu ambazo ni Kifaru Sekondari,Kileo Sekondari na Shule ya Sekondari ya wavulana ya Mt.Joseph ambayo ni ya binafsi.Kata ya Kileo ina Zahanati mbili,Zahanati ya Kileo na Zahanati ya Kifaru.Wananchi wa kata ya Kileo wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara,ufugaji wa ng'ombe,mbuzi,kondoo,kuku;pamoja na biashara ndogo ndogo.

### 2.0 .ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari.

### 3.0.VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA

Katika kipindi hiki,vikao na mikutano ya kisheria ilifanyika kama ifuatavyo:-

3.1.VIKAO VYA WDC/KMK

| Na. | LENGO | HALISI | MENGINEYO/MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | |

3.2.VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI

| Na. | KIJIJI | VIKAO | | MIKUTANO | | MENGINEYO/MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Lengo | Halisi | Lengo | Halisi | |
| 1 | Kifaru | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| 2 | Kileo | 3 | 2 | 1 | 0 | Akidi haitimii |
| 3 | Kituri | 3 | 2 | 1 | 1 | |
| 4 | Kivulini | 3 | 2 | 1 | 0 | Akidi haikutimia kwa ajili ya mkutano |

### 3.3.MIKUTANO YA WAKAZI WA VITONGOJI

| Na. | KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO/MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kifaru | 4 | 12 | 12 | |
| 2 | Kileo | 5 | 15 | 15 | |
| 3 | Kituri | 4 | 12 | 12 | |
| 4 | Kivulini | 4 | 12 | 12 | |

## 4.0. TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI ZILIZOSOMWA KWENYE MIKUTANO MIKUU YA VIJIJI

### 4.1.Mapato yaliyosomwa kwenye mikutano mikuu ya Vijiji

Kwa kipindi cha robo ya kwanza taarifa za mapato na matumizi zilisomwa na kukubalika kwenye mikutano mikuu ya vijiji vya kata ya Kileo kama ifuatavyo:-

| Na. | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO/MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kifaru | 1 | 1 | |
| 2 | Kileo | 1 | 0 | |
| 3 | Kituri | 1 | 1 | |
| 4 | Kivulini | 1 | 0 | |
| | **Jumla** | **4** | 2 | |

### 4.2.Mapato ya Halmashauri ya Wilaya

#### 4.2.1Ukaguzi na usafi wa nyama

| Na. | Aina | Idadi | @ | Tsh |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 77 | 1,500/= | 115,500/= |
| 2 | Mbuzi | 60 | 800/= | 48,000/= |
| 3 | Kondoo | 105 | 800/= | 84,000/= |
| JUMLA | | | | 247,500/= |

## 5.0.MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA

### 5.1.Miradi ya Maendeleo

Katika kipindi cha robo ya kwanza miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

| KIJIJI/ TAASISI | MRADI | THAMANI | CHANZO CHA FEDHA | HATUA ILIYOFIKIWA |
|---|---|---|---|---|
| Kijiji cha Kifaru | Ujenzi wa shimo la Choo cha ofisi | Tsh.1,373,000/= | Mapato ya kijiji | Kazi imekamilika |
| Kifaru Sekondari | Kuweka vioo kwenye jingo la maabara | Tsh.527,000/= | Elimu bure | Kazi imekamilika |
| Kivulini | Kuweka mfumo wa solar kwenye pump ya maji shule ya msingi Kivulini/Mkombozi | Tsh.42,000,000/= | Mfadhili | Kazi imekamilika |

### 5.2.Taarifa za Kisekta

**Elimu**

-Vyumba viwili vya madarasa vya shule ya Msingi Kifaru yanahitaji kujengewa gebo na hakuna choo cha walimu

-Wanafunzi wane wa Kifaru Sekondari wamebainika kuwa wajawazito na wamefuzwa shule.

-Idadi ya wanafunzi wanaopata chakula cha mchana shuleni Kifaru Sekondari imeongezeka.

-Utoro wa wanafunzi Kifaru Sekondari umeongezeka

**Mifugo**

- Mipango ya Ukarabati wa josho inaendelea.
- Zoezi la kuua mbwa wazururaji limeendelea kwani mbwa hao ni hatari kwa usalama wa raia.

**Afya**

- Hapakutokea magonjwa ya mlipuko.
- Kuna ongezeko la ujenzi na matumizi ya vyoo bora.
- Elimu imetolewa kwa wafanyabiashara wasichanganye bidhaa za vyakula na dawa,sumu na pembejeo.
- Dawa muhimu zinapatikana kwenye zahanati zetu zote.

## 6.0.CHANGAMOTO NA NAMNA/MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO KWA UJUMLA

### 6.1.Changamoto

- Wananchi hawahudhurii vikao na mikutano ya kisheria.
- Kuna upungufu wa walimu 16 wa shule za msingi katika kata ya Kileo.

### 6.2.Mikakati ya kukabiliana na Changamoto

- Sheria za vijiji zitumike kuwawajibisha wananchi wasiohudhuria vikao.
- Taarifa imekwishatolewa kwa Afisaelimu Msingi kuhusu upungufu wa walimu.

Nawasilisha.

……………

Mwenyekiti

……………

Katibu

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA MAENDELEO KATIKA KATA YA JIPE KWA ROBO YA PILI KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 14/11/2017.

## UTANGULIZI:-

Kata hii inaundwa na vijiji vitatu (3) ambavyo ni Jipe,Kambiyasimba na Butu Ugweno.

Kata hii imepakana na nchi jirani ya Kenya Upande wa Mashariki, Magharibi imepakana na Tarafa ya Ugweno, Kusini imepakana na Kata ya Kigonigoni na kaskazini imepakana na kata ya Kivisini.

## HALI YA USALAMA:-

1. Kwa kipindi hiki hali ya usalama ilikua sio nzuri kwani kulitokea matukio mawili ambayo yalisababisha upotevu wa maisha.
   a. Kijiji cha Kambiyasimba nyumba moja iliungua moto, mtoto mmoja alipoteza maisha.
   b. Kijiji cha Butu Ugweno kijana mmoja alizama ndani ya ziwa Jipe na kupoteza maisha. na mtoto huyo ni wa M.Diwani Mkono
2. Uhusiano kati ya wakulima na wafugaji ni mzuri.
3. **Mazingira:-** katika kata ya jipe agizo la Mh. Raisi linatekelezwa kwa kufanya usafi kila jumamosi ya mwisho wa mwezi(zoezi hili ni endelevu)
4. **Uhamiaji haramu:-** kwa kipindi hiki hakuna wahamiaji haramu

**Vikao vya kisheria (wdc)**

| Kata | Lengo | Halisi | Mengineyo |
|---|---|---|---|
| Jipe | 1 | 1 | |

Vikao vya kisheria vya vijiji

| Kijiji | Lengo | Halisi | Mengineyo |
|---|---|---|---|
| Jipe | 3 | 0 | Taarifa yake haikusomwa |
| Kambiyasimba | 3 | 1 | |
| Butu – ugweno | 3 | 3 | |

**Mikutano mikuu ya kisheria ya vijiji:- mapato na matumizi**

| Kijiji | Lengo | Halisi | Mengineyo |
|---|---|---|---|
| Jipe | 1 | 0 | |
| Kambiyasimba | 1 | 0 | |
| Butu – ugweno | 1 | 1 | |

VIONGOZI

1. JIPE HAWAKUFAA-IA
2. K/SIMBA KITI 2
3. BUTU vimechaa 4

**MAPATO YA HALMASHAURI**

1. Jipe:- ushuru wa mazao = 100,000/=
2. Kambiyasimba:- ushuru wa nyama = 10,000/=
3. Butu:- ushuru wa samaki 20,000/=

   Jumla ya mapato = 130,000/=

## TAARIFA ZA KISEKTA

**ELIMU:-** kata ina shule za msingi tatu Jipe,Kambiyasimba na shule ya msingi Butu. Pia kata ina shule ya sekondari moja nayo ni shule ya sekondari JIPE ambayo ilipata fedha za mfuko wa LCDG Tsh 19,830,400/= kwa ajili ya umaliziaji wa nyumba ya watumishi. Kazi zilizofanyika ni umaliziaji wa gebo na upauzi tuu. Shughuli za ujenzi zimesimama kwasababu hakuna muweka saini Benki baada ya mtendaji wa kijiji kusitishwa ajira yake. Hivyo tunaomba tupatiwe mtendaji wa kijiji haraka ili fedha hizo zisikatwe na benki kila mwezi.

**ELIMU YA MSINGI:-**

Chakula cha mchana kwa kipindi hiki ni shule moja tuu ya msingi Jipe ndio watoto wanakula chakula cha mchana – **WDC** imekaa na kuwaagiza viongozi wa vijiji Butu na Kambiyasimba wasimamie zoezi hilo la wanafunzi kupata chakula mashuleni.

**AFYA:-** Kata ya Jipe ina Zahanati tatu Jipe, Kambiyasimba na Butu.

I.C.H.F – Kwa kipindi hiki kata ya Jipe imekusanya Tsh. 875,000/=

JIPE waliojiunga ni kaya 8 = 240,000

Papo kwa papo ni 7 = 42,000

BUTU waliojiunga ni kaya 6 = 180,000

Papo kwa papo ni 0

KAMBIYASIMBA waliojiunga ni kaya 13 = 390,000/=

Papo kwa papo 7 = 42,000/=

**MAJI:** kwa kipindi hiki kata ya Jipe inaupungufu mkubwa wa maji haswa kijiji cha Jipe pamoja na wanafunzi wa sekondari. Shule imepata mfadhili wa kuchimba maji ya ardhini lakini maji yaliyopatikana hayafai kwa matumizi ya kibinadamu. Utafiti wa kupata eneo linguine litakalotoa maji mazuri unaendelea.

**KILIMO:-** katika kata ya Jipe hali ya chakula sio nzuri kutokana na mvua za masika kutonyesha za kutosha. Wananchi wanaupungufu mkubwa wa chakula. Kwa sasa hivi wananchi wanaotesha mazao ya chakula baada ya mvua za vuli kuanza kunyesha.

**UVUVI:-** wananchi wa kata ya Jipe kuna wanajishughulisha na uvuvi kwa kutega, lakini limeibuka kundi la wavuvi wanaovua kwa kutumia zana haramu, zoezi la kuwakamata limefanyika na zimekamatwa nyavu haramu kumi na zimeteketezwa kwa kuchomwa moto. Viongozi wa vijiji na wilaya wanaendelea kutoa elimu kuhusu uvuvi haramu na wakaidi wataendelea kuchukuliwa hatua kali.

**MIFUGO:-** kwa kipindi hiki hakuna magonjwa ya milipuko ila kuna uhaba wa majani na kwa sasa hivi zoezi linaloendelea ni kuhamasisha chanjo ya kichaa cha Mbwa.

**MAENDELEO YA JAMII:-**

Kata ya Jipe ina SACCOS moja NGUVUMALI SACCOS L.T.D ambayo inatoa mikopo kwa jamii na inahudumia kata za Jipe,Kivisini na kata ya Kigonigoni na kipindi hiki imetoa gawio la faida kwa wanachama wake. Pia tunaishukuru Halmashauri ya wilaya kwa kuwapatia mikopo vikundi viwili

vya vijana kijiji cha Jipe na Kambiyasimba. Tunaomba vikundi vya wanawake navyo vifikiriwe kupatiwa mikopo hiyo.

<u>CHANGAMOTO:-</u>

1. Upungufu wa watendaji wa vijiji - Jipe na Kambiyasimba.
2. Upungufu wa watumishi wa Zahanati.
3. Upungufu wa wataalamu wa kilimo na mifugo.
4. Upungufu wa watumishi wa maendeleo ya jamii.
5. Upungufu mkubwa wa chakula.

Naomba kuwasilisha.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA KIRYA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA 2017

### 1. UTANGULIZI

Kata ya Kirya inapakana na kata ya Lang'ata upande wa kaskazini, Kusini kuna kata ya Ruvu Muungano wilaya ya Same, Mashariki imepakana na Kata ya Lembeni na Mgagao, Magharibi inapakana na Kata ya Ngorika wilaya ya Simanjiro mkoa wa Manyara.

### 2. UTAWALA

Kata ya Kirya imeundwa na vijiji vitatu ambavyo ni Kirya, Njiapanda na Kiti Cha Mungu, ina jumla ya vitongoji saba.

### 3. ELIMU

Kata ina sekondari moja ya Kirya na ina shule nne za msingi ambazo ni Kirya, Emangulai, Kiti cha Mungu na Dr. Omary.

### 4. AFYA

Kata ina zahanati tatu ambazo ni Kirya, Njiapanda na Kiti cha Mungu

### 5. NJIA ZA UCHUMI KWA WANANCHI

Njia kuu za uchumi katika kata hii ni kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara ndogondogo

### 6. ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama ni ya wastani

### 7. (i) VIKAO VYA WDC

| KATA | LENGO | KIMEFANYIKA | HAKIKUFANYIKA |
|---|---|---|---|
| KIRYA | 1 | 1 | 0 |

(ii)VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI

| VIJIJI | VIKAO | | MIKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| KIRYA | | | | | Taarifa za kijiji hazijaletwa wala kujadiliwa na WDC |
| NJIAPANDA | 3 | 2 | 1 | 0 | |
| KITI CHA MUNGU | 3 | 3 | 1 | 0 | |

(iii) MIKUTANO YA WAKAZI WA KITONGOJI

| KATA | KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI |
|---|---|---|---|---|
| | KIRYA | 3 | 9 | Haijafanyika |
| KIRYA | NJIAPANDA | 2 | 6 | 5 |
| | KITI CHA MUNGU | 2 | 6 | 2 |
| | | | | |

8. MAPATO NA MATUMIZI

(i)TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ZILIZOSOMWA KWENYE MIKUTANO YA VIJIJI

| KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIRYA | | | Taarifa za kijiji hazijaletwa kwenye WDC |
| NJIAPANDA | 22,000,000 | 5,703,000 | |
| KITI CHA MUNGU | 6,000,000 | 1,595,000 | |

(ii) MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA

| KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIRYA | | 330,000 | Mapato haya ni ya ushuru wa mazao taarifa imesomwa na afisa kilimo wa kata |
| NJIAPANDA | ---------- | 635,000 | |
| KITI CHA MUNGU | ---------- | 174,000 | |

(iii) MAPATO YA HALMASHAURI YA VIJIJI

| KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIRYA | | | |
| NJIAPANDA | 22,000,000 | 5,703,000 | |
| KITI CHA MUNGU | 6,000,000 | 1,595,000 | |

9. MAKUSANYO YA BIMA YA AFYA ILIYOBORESHWA

| KIJIJI | IDAD YA WANACHAMA | KIASI CHA FEDHA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIRYA | 14 | 420,000 | |
| NJIAPANDA | 7 | 210, 000 | |
| KITI CHA MUNGU | 1 | 30,000 | |

10.TAARIFA ZA KISEKTA

1. ELIMU

   Sekondari ya Kirya haina walimu wa sayansi kabisa na shule zote nne za msingi zina upungufu mkubwa wa walimu. Shule zote zina maendeleo mazuri kitaaluma.

2. AFYA

   Muitikio wa elimu ya mazingira ni mdogo sana hivyo usafi wa mazingira na vyoo kutofanyika kwa kiwango cha kuridhisha

3. MIFUGO

   Hali ya mifugo ni shwari kiasi, kumekuwa na mlipuko wa magonjwa uliosababisha Ngo’mbe 35, Mbuzi 233, Kuku 64 na Mbwa 1 kufa.

4. UVUVI

   Uvuvi haramu bado upo hasa kijiji cha Njiapanda na Kiti cha Mungu. Doria zilifanyika na vyandarua viwili viliteketezwa kwa moto.

5. KILIMO

Hali ya mazao ni nzuri. Mazao yaliyopandwa kipindi hiki ni mahindi, mpunga na mbogamboga.

10. CHANGAMOTO NA NAMNA ZILIVYOKABILIWA

(i) Upungufu mkubwa wa walimu

Wazazi wanachanga pesa kuwalipa walimu wa ziada

(ii) Ugomvi wa wakulima na wafugaji na uhalibifu wa miundombinu ya umwagiliaji mashambani

Hatua za kisheria zimechukuliwa, vikao vya maridhiano pia vimefanyika

(iii) Ubovu wa lambo na ukosefu wa josho la mifugo

Changamoto hii bado haijatatuliwa

MAPENDEKEZO/ MAOMBI

Kata ya Kirya inatoa mapendekezo/ maombi kama ifuatavyo;

- Halmashauri kuleta mzabuni wa ukusanyaji ushuru au mapato ya samaki na mazao ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya wilaya.
- Kuajiri na kuwapangia vituo watendaji wa vijiji vya kiti cha Mungu na Kirya
- Fedha za vijiji kuwekwa kwennye akaunti zao kwa wakati
- Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na josho la ~~migugo~~ mifugo

**NAOMBA KUWASILISHA**

**KATIBU** **MWENYEKITI**

# HALMASHAURI WILAYA YA MWANGA KATA YA KIGHARE

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAENDELEO KATA YA KIGHARE KUANZIA JULY-SEPT 2017. ( ROBO YA KWANZA)

### i) UTANGULIZI

Kata ya Kighare imepakana na Kata ya Msangeni na Shighatini kwa upande wa kaskazini. Kusini imepakana na Kirongwe na Chomvu, Mashariki Kata ya Kirongwe na Magharibi Kata ya Ngujini na sehemu ya Shighatini.

Kata hii imeundwa na vijiji vinne na vitongoji kumi na nane (8).

Kata ya Kighare ina idadi ya watu 6254 kwa sensa ya makazi na watu ya mwaka 2012. Kati ya hao wanawake ni 3339 na waliobaki wanaume.

### ii) TAASISI ZA ELIMU NA AFYA

**a) ELIMU:-**

Shule za msingi zipo sita (6), ambazo ni Kiriki, Kavazungu, Kwamsembea, Katola, Kilaweni, na Kamwala.

Shule za sekondari ni moja tu ya serikali ambayo ni Kighare na binafsi ni Kiriki.

Aidha kuna chuo kimoja cha ufundi ( UVTC)

**b) AFYA**

Kata ya Kighare kuna zahanati tatu ambazo ni Ndanda, Kighare na Kirongaya. Aidha ipo hospitali ya Wilaya ambayo ni Usangi katika Kijiji cha Kilaweni

### iii) NJIA KUU ZA UCHUMI

Wananchi wa Kata hii wanategemea kilimo cha mchanganyiko ( mseto), Ufugaji wa ndani na biashara ndogo ndogo.

### 2. ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama katika Kata hii ni wa wastani kwani kuna wizi wa hapa na pale wa mazao kama ndizi na kuku. Tunaamini suluhuhisho litapatikana tutakapofanikiwa kuwa na kituo cha polisi katika Tarafa ya Usangi.

### 3. VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA

**i) Ngazi ya Kata**

| KATA | LENGO | HALISI | MAONI |
|---|---|---|---|
| KIGHARE | 1 | 1 | - |
| | | 2 | |

**ii) Ngazi ya Kijiji**

| | HALMASHAURI | | MIKUTANO | | |
|---|---|---|---|---|---|
| JINA KIJIJI | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
| KILAWENI | 3 | 2 | 1 | 1 | |
| KIGHARE | 3 | = | 1 | = | |
| KIRONGAYA | 3 | 2 | 1 | = | |
| NDANDA | 3 | - | 1 | - | |

**Iii ) Ngazi ya Vitongoji**

| KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| KILAWENI | 03 | 9 | 1 | - |
| KIGHARE | 5 | 15 | 02 | - |
| KIRONGAYA | 4 | 12 | - | - |
| NDANDA | 6 | 18 | - | - |

**MAPATO YA HALMASHAURI**

Kipindi cha robo ya kwanza 2017

| MWEZI | MAPATO YA LESENI | USHURU WA NYAMA |
|---|---|---|
| JULY | 20,000/= | 34,500/= |
| AUGUST | 3,OOO/= | 52,500/= |
| | (FAINI UHARIBIFU WA MAZINGIRA) | |
| SEPTEMBER | - | 45000/= |
| JUMLA | | 132,000/= |

**4. MIRADI YA MAENDELEO YA KISEKTA**

i) Michango ya wanachama wa CHF robo ya kwanza ( July – Sept) – Hospitali ya Usangi.

| MWEZI | AINA YA MAPATO | | WANACHAMA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | CHF | PAPO KWA PAPO | | |
| JULY | 640000/= | 140,000/= | 64 | 780,000/= |
| AUGUST | 880000/= | 2110,000/= | 88 | 1000,000/= |
| SEPTEMBER | 530000/= | 270,000/= | 53 | 800,000/= |
| JUMLA | 2050000/= | 620,000/= | 205 | 2670,000/= |

**ii) ZAHANATI YA NDANDA CHF**

| MWEZI | AINA YA MAPATO | | WANACHAMA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | CHF | PAPO KWA PAPO | | |
| JULY | 80 | - | 08 | 80,000/= |
| AUGUST | 100.000/= | - | 10 | 100,000/= |
| SEPTEMBER | 100,000/= | - | 11 | 110,000/= |
| JUMLA | 290,000/= | - | 29 | 290,000/= |

**<u>Iii)</u> ZAHANATI YA KIGHARE. CHF**

| MWEZI | AINA YA MAPATO | WANACHAMA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| JULY | 20,000/= | 2 | 20,000/= |
| AGUST | 50,000/= | 5 | 50,000/= |
| SEPTEMBER | 110,000/= | 11 | 110,000/= |
| JUMLA | 180,000/= | 18 | 180,000/- |

## ZAHANATI YA KIRONGAYA

| MWEZI | AINA YA MAPATO | | WANACHAMA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | CHF | PAPO KWA PAPO | | |
| JULY | 80,000/= | - | 8 | 80,000/= |
| AUGUST | 70,0000/= | - | 7 | 70,000/= |
| SEPTEMBER | 80,0000/= | - | 8 | 80,000/= |
| JUMLA | 230,000/= | - | 23 | 230,000/= |

## TAARIFA ZA IDARA YA MIFUGO

Wafugaji waliotembelewa na kupewa ushauri nasaha.

| MWEZI | KILAWENI | | KIGHARE | | KIRONGAYA | | NDANDA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE |
| JULY | 4 | 12 | 12 | 09 | 12 | 18 | 24 | 2 |
| AUGUST | 90 | 72 | 36 | 84 | 15 | 14 | 16 | 2 |
| SEPT | 21 | 11 | 10 | 8 | 37 | 47 | 76 | 96 |
| JUMLA | 115 | 95 | 58 | 101 | 64 | 81 | 116 | 100 |

Jumla ya wafugaji 771 walitembelewa na kupewa ushauri

## TAARIFA YA IDARA YA KILIMO

Hali ya chakula katika Kata ni ya kuridhisha bei zimepungua kulinganisha na kipindi kilichopita.

Bei ya mazao katika Kata ya Kighare JULY – SEPTEMBER 2017

| ZAO | JULY- TSHS | AUGUST | SAPT |
|---|---|---|---|
| Maharage | 2500 @ kg | 2500/= | 2400/= |
| Mahindi | 800/= | 800/= | 700/= |
| Kunde | 1800/= | 1800/= | 1600/= |
| Nyanya | 5000 sado | 5000/= | 5000/= |
| Vitunguu | Sado 5000/= | 5000/= | 4000/= |
| Kabichi | Fungu 800/= | 800/= | 500/= |
| Mchicha | Fungu 300/= | 300/= | 300/= |
| Magimbi | Fungu 1000/= - | 1000/= | 1000/= |
| Viazi vitamu | Fungu 1000/= | 1000/= | 1000/= |
| Ndizi | Mkungu 6000/= | 6000/= | 6000/= |

**ELIMU**

**UFAULU WA WANAFUNZI S/MSINGI 2017**

| SHULE | IDADI YA WATAHINIWA | WALIOFAULU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| KIRIKI | 15 | 14 | 93% |
| KAVAZUNGU | 17 | 17 | 100% |
| KWAMSEMBEA | 28 | 20 | 71% |
| KATOLA | 20 | 19 | 95% |
| KILAWENI | 22 | 22 | 100% |
| KAMWALA | 19 | 15 | 79% |
| JUMLA | 121 | 107 | 88% |

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KATA**

i) Uhaba wa watendaji wa vijiji na Kata. Mikutano na vikao vya halmashauri za vijiji hazijafanyika kutokana na uhaba.

ii) Bado makabidhiano ya ofisi ya Kijiji cha Ndanda hayajafanyika hivyo hakuna mapato ya Kijiji.

iii) Uharibifu wa mazingira unaotokana na watu kukata miti hovyo na watendaji na kuwawajibisha kutokuwepo.

iv) Wanyama waharibifu katika Kijiji cha Kighare – kwa magire na Ndanda wamekuwa tishio kwa wakulima.

v) Miradi ya ofisi ya Kijij cha Kilaweni, jengo la mganga- Kirongaya na zahanati ya Kilaweni yamesimama na yanaendelea kuharibika kwani Mkurugenzi anatakiwa ayapaue.

**MAPEMDEKEZO**

i) Tunaomba kupatiwa watendaji wa Vijiji vyote na Kata mapema iwezekanavyo.

ii) Tunaomba ofisi ya Mkurugenzi iweke kipaumbele kwenye kukamilisha upauzi na ujenzi wa majengo tajwa hapo juu ili nguvu za wananchi zisipotee bure.

Naomba kuwasilisha

Mbaga

…………………………..
Mh. Diwani- Kighare

…………………………..
Afisa mtendaji Kata

AFISA MTENDAJI KATA YA KIGHARE

## TAARIFA YA MAENDELEO YA KATA YA KIFULA KUANZIA JULY – SEPTEMBA 2017 TAR. 14/11/2017

**SEHEMU YA PILI.**

**UTANGULIZI**

I. **MIPAKA.**

Kata ya kifula inapakana na kata ya Mwaniko upande wa kaskazini Mashariki inapakana na kata ya Jipe na Magharibi Kata ya Msangeni Kusini Kata ya Kigonigoni.

II. **UTAWALA.**

Kata ya Kifula inaundwa na vijiji vitano ambavyo ni:- Raa,Kadengere, Kisanjuni, Rangaa na Masumbeni vyenye jumla ya vitongoji 19.

III. **ELIMU.**

Kata ya KIfula ina shule za msingi 7 nazo ni:- Raa, Rangaa, Masumbeni, Kifula, Mbore, Fumbuang'ombe na Kisanjuni. Sekondari mbili:- Mijna ya wazazi na Kishengweni secondary ya kutwa.

IV. **AFYA.**

Kata ya Kifula ina Zahanati moja iitwayo Raa na Kituo cha afya kimoja kiitqwacho Kifula.

V. **UCHUMI.**

Njia kuu ya uchumi kwa wananchi wa kata ya Kifula ni Kilimo, Ufugaji wa ng'ombe wa ndani na biashara ndogondogo.

**SEHEMU YA TATU**

**HALI YA ULINZI NA USALAMA.**

Hali ya ulinzi na usalama katika vijiji vya kata ya Kifula ni shwari.

**SEHEMU YA NNE.**

**VIKAO VYA MKUTANO MKUU.**

| VIKAO | | | MIKUTANO MIKUU | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KAYA NA VIJIJ | LENGO | HALISI | | LENGO | HALISI |
| WDC | 1 | 1 | | | |
| RANGAA H/KIJIJI | 3 | 1 | RANGAA | - | - |
| RAA H/KIJIJI | 3 | 3 | RAA | 1 | 1 |
| KADENGERE H/KIJIJI | 3 | 3 | KADENGERE | 1 | 1 |
| MASUMBENI H/KIJIJI | 3 | 1 | MASUMBENI | - | - |
| KISANJUNI H/KIJIJI | 3 | 1 | KISANJUNI | - | - |

Vitongoji Kadengere Halisi 3 → 2
Kisanjuni Halisi 3 – 2

**SEHEMU YA TANO**
**MAPATO YA H/WILAYA**
**ADA YA UKAGUZI WA NYAMA YA NG'OMBE**

| MWEZI | LENGO | HALISI |
|---|---|---|
| July | | 39000 |
| October | | 45000 |
| September | | 49500 |
| **JUMLA** | | **133500** |

**MAPATO YA CHF**

Zaanati ya Raa

| | |
|---|---|
| July | |
| 8 | |
| September | |

Kituo cha afya

| | |
|---|---|
| July | |
| 8 | |
| September | |

Ada ya leseni kijiji cha Raa Tsh 49000
-II – II – Masumbeni 21000
-II-II- Kadengere 21000
-II-II- Kisanjuni 121000
Ushuru wa soko kijiji cha Kisanjuni tsh 3685000
**JUMLA 580500**

**UHAMIAJI HARAMU**

Uhamiaji haramu hakuna.

**SAHEMU YA SITA**

**MIRADI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA**

**ELIMU.**:- Wananchi wameendelea kuhamasishwa kuchangia fedha kwa ajili ya chakula cha mchana shuleni pia elimu ya wanafunzi kujiunga na mfuko wa Bima ya afya ilivyoboreshwa imeendelea kutolewa katika vikao vya kamati za shule, mabaraza ya wanafunzina mikutano ya wazazi shuleni.

**KILIMO.**
**SHUGHULI ZILIZOFANYIKA.**

Wananchi wameelimishwa kuandaa mashimo na mbolea kwa ajili ya kupanda kahawa za kisasa ambazo hazitahitaji dawa za sumu.

**MAZINGIRA.**

Kata ya Kifula inakabiliwa na tatizo la miti aina ya Agrocaps iliyopandwa karibu na vyanzo vya maji na imesababisha vyanzo vingi vya maji kukauka. Tumeorodhesha majina ya watu waliopanda miti hii pia tumewashauri waondoe miti hiyo wamekubali wanang ojea kupewa kibali cha kuivuna. Kupitia kikao hiki tunaomba waruhusiwa kuivuna hiyo miti.

**SEHEMU YA SABA**

**MAFANIKIO NA CHANGAMOTO NA NAMNA YA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO KWA UJUMLA NA MAFANIKIO**

| | | |
|---|---|---|
| NDIZI | 2.0 Tani | 2000 kg |
| MCHICHA | 1.0 Tani | 1000 kg |
| MAGIMBI | 0.2 Tani | 200 kg |
| CHAINIZI | 0.1 Tani | 100 kg |

**CHANGA MOTO**

- Mvua zimenyesha
- kidogo zimesababisha mimea kudumaa
- Ofisi za vijiji kutofunguliwa kwa wakati
- Vikao na mikutano kushindikana kufanykika , kukwama miradi ya maendeleo kuendelea

**MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

- Wananchi wameelimishwa kutunza chakula kilichopo
- Halimashauri ya Wilaya iajiri watendaji wa vijiji na vijiji vya Masumbeni, Kisanjuni na Rangaa vipate watendaji wa kudumu.

**HITIMISHO.**

Mheshimiwa mwenyekiti naomba baraza lako tukufu lipokee taarifa hii na kuijadili pia itoe ushauri kwa faida ya kamati ya maendeleo kataya Kifula.

Imeandaliwa na kuratibiwa na

**Mw/kiti kamati ya maendeleo kata ya Kifula** **Katibu**

AFISA MTENDAJI KATA
KATA YA KIFULA
MWANGA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA SHIGHTINI JULY- SEPTEMBER 2017

**SEHEMU YA 2**

Kata ya Shightini ni miongoni mwa kata zilizomo katika Halmashauri ya wilaya ya Mwanga. Kata hii imepakana na kata ya kighare upande wa mashariki, kata ya Mwanga upande wa magharibi, kat ya Ngujini upande wa kusini na kaskazini imepakana na kata ya Msangeni.

**UTAWALA**

Kata ya Shighatini ina jumla ya vijiji sita vinavyofanya kazi na shughuli zote za kiutendaji ambavyo ni:- **SHIGHATINI, MFINGA, MKUU, VUCHAMA NDAMBWE, IBAYA NA LAMBO.**Na pia kata ina jumla ya vitongoji ishirini na moja

**ELIMU**:- Kata ina shule za msingi saba na shule za sekondari tatu moja ikiwa ni ya binafsi na ujenzi wa shule ya sekondari ya nne ya Ngolea kijiji cha Lambo unaedelea. Pia kuna upungufu wa walimu mkubwa hasa katika shule za msingi.

**AFYA** :Kata ina jumla ya zahanati tano ambazo ni:-

- Lambo
- Ibaya
- Mfinga
- Mkuu
- Vuchama ndambwe
- kituo teule cha afya kimoja Shightini.

Hata hivyo mpango wa ujenzi wa kituo cha afya umeanza ndani ya kata na uwanja umekamilika kwa sehemu kubwa katika kijiji cha mfinga.

**NJIA KUU YA UCHUMI WA WANANCHI KATIKA KATA**;- Kilimo na mifugo

**SEHEMU YA 3**

**ULIZI NA USALAMA :- HALI YA ULINZI NA USALAMA KATIKA KATA**

Hali ya usalama ni shwari hakuna tukio lolote baya lililotokea katika kata.

**SEHEMU 4**

**VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA, VIJIJI NA VITONNGOJI:-**

(1)JEDWALI "A'' VIKAO WDC

| NA | KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 1 | |

## (2) JEDWALI "B" VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA YA KIJIJI

| NA | KATA | KIJIJI | VIKAO | | MIKUTANO | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| | SHIGHATINI | MKUU | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | IBAYA | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | SHIGHATINI | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | V/NDAMBWE | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | LAMBO | 3 | 3 | 1 | 1 | |
| | | MFINGA | 3 | 2 | 1 | 1 | |
| | | | | | | | |

## (3) JEDWALI "C" MIKUTANO YA WAKAZI WA VITONGOJI.

| NA | KATA | KIJIJI | IDADI YA VITONGOJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SHIGHATINI | MKUU | 3 | 9 | 0 | |
| | | IBAYA | 3 | 9 | 0 | |
| | | SHIGHATINI | 3 | 9 | 3 | |
| | | V/NDAMBWE | 3 | 9 | 0 | |
| | | LAMBO | 6 | 18 | 6 | |
| | | MFINGA | 3 | 9 | 0 | |
| | | | | | | |

## MIGOGORO YA ARDHI NA MIPAKA

Kata ya Shightini ina migogoro ya mipaka katika vijiji vya Mkuu na Vuchama Ndambwe Shightini na Ibaya. Hata hivyo hoja ya kupatiwa wataalamu ili kubaini uhalali wa mipaka kwa kila kijiji ni ya msingi ili kuondoa migogoro hiyo.

## KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:

Hali ya chakula ni wastanii;bei ya chakula mahindi 11,500/=@debe,maharage 2500/=@kilo
Wakulima wanashauriwa kuendelea kuhifadhi chakula.Kila kaya ihakikishe inahifadhi chakula chakutosha.

**Maandalizi ya kilimo cha Vuli**;Maanalizi ni mazuri,wakulima wengi wamejitokeza kulima mashamba yao.Wakulima wameitikia kuandaa mbegu bora mapema na mbolea za kupandia kama vile DAP/NPK/FYM (Samadi).Mvua za vuli zimeanza na hadi sasa wakulima wameotessha mahindi na kg 1500 za mbegu zimeshauzwa.

**Ufufuaji wa zao la kahawa;**ufufuaji unaendelea **kwa msimu huu** tunategemea kuotesha miche bora ya kahawa zaidi ya 2500ndani ya kata..Kuna upungufu wa Maafisa ugani 4.

**MIFUGO**

1 .Taarifa ya makusanyo ,katika kipindi cha Julyl-September 2017 tumekusanya shilling 95,300/=Kwa mchanganuo ufuatao ngombe 63 T.shs 94,500/=na kondoo 1 T.shs 800/=

2.Kipindi cha September kulikuwa na uhaba wa malisho.Hali ya mifugo siyo mbaya,hapakutokea magonjwa ya mlipuko.

**SEHEMU YA 5**

**MAPATO NA MATUMIZI**

1 .TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI ZILIZOSOMWA KWA BAADHI YA VIJIJI KWENYE MIKUTANO MIKUU YA VIJIJI

Kwa kipindi cha Robo ya kwanza .Taarifa za mapato na matumizi zilisomwa na kukubalika kwenye mikutano mikuu ya vijiji vya Kata ya Shighatini kama ifuatavyo:-

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MKUU | 1 | 1 | |
| 2 | IBAYA | 1 | 1 | |
| 1 | SHIGHATINI | 1 | 1 | |
| 4 | V/NDAMBWE | 1 | 1 | |
| | LAMBO | 1 | 1 | |
| 6 | MFINGA | 1 | 1 | |

**2. MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA.**

Kwa kipindi cha robo ya kwanza, Vijiji vya Kata ya Shighatini vilikusanya mapato ya Halmashauri ya wilaya kama inavyoonekana hapa chini:

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MKUU | | - | |
| 2 | IBAYA | | - | |
| 3 | SHIGHATINI | | 117,000/= | |
| 4 | V/NDAMBWE | | 63,000/= | |
| 5 | LAMBO | | 94,000/= | |
| 6 | MFINGA | | - | |

| Makusanyo Katika Machinjio July-september2017 | NG'OMBE 63 | KONDOO 1 | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | Tsh.94,500,000.00 | Tsh.800.00 | Tsh.95,300 |

**3. MAKUSANYO YA HALMASHAURI ZA VIJIJI.**

Mapato ya Halmashauri za vijiji vya kata ya Shighatini yaliyokusanywa kama ifuatavyo:-

| NA | KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MKUU | | - | |
| 2 | IBAYA | | - | |
| 3 | SHIGHATINI | | - | |
| 4 | V/NDAMBWE | | 33,000/= | |
| 5 | LAMBO | | - | |
| 6 | MFINGA | | - | |

**4. MAKUSANYO YA CHF KWENYE VITUO – JULY – SEPTEMBER – 2017**

| NA. | KIJIJI | PAPO KWA PAPO (CHF) | iCHF | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Lambo | | 150,000/= | 150,000/= |
| 2 | Ibaya | | 165,000/= | 165,000/= |
| 3 | Mfinga | | 48,000/= | 48,000/= |
| 4 | Vuchama Ndambwe | | 150,000/= | 150,000/= |
| 5 | Mkuu | 18,000/= | - | 18,000/= |
| 6 | Shighatini | | - | - |
| | **Jumla** | | | |

**<u>5.MIRADI YA TASAF – III – MPANGO WA KUNUSURU KAYA – MASKINI. JULY-AUGAST, SEPTEMBER-OCTOBER</u>**

| No. | KIJIJI | MAPOKEZI YA FEDHA KWA WALENGWA | ASILIMIA 1.5% | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Vuchama Ndambwe | 4,168,000.00 | 200,000.00 | 4,368,000.00 |
| 2 | Mfinga | 1,196,000.00 | 200,000.00 | 1,396,000.00 |
| 3 | Lambo | 6,284,000.00 | 200,000.00 | 6,484,000.00 |
| 4 | Mkuu | 2,064,000.00 | 200,000.00 | 2,264,000.00 |
| 5 | Shighatini | 4,008,000.00 | 200,000.00 | 4,208,000.00 |

**SEHEMU YA 5**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI YA MAENDELEO KIPINDI CHA JULY – SEPTEMBER 2017 KATA YA SHIGHATINI.**

| NA | ENEO LA MRADI | AINA YA MRADI | KAZI ZILIZO FANYIKA | NGUVU KAZI | THAMANI/ GARAMA ZA | UCHANGI AJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | H/WILAYA | WAHISANI |
| | VUCHAMA NDAMBWE | 1.Ujenzi wa jengo la utawala S/Msingi Ndambwe | • Kumalizia ukarabati wa kuta na upauaji wa jengo | 325,000/= | | |
| | | 2.Kukamilika kwa bweni moja na linguine lipo hatua ya lenta pamoja na madara manne | • ujenzi | 8,000,000/= | Serikali kuu milioni 259,000,000/= | |
| | | 3.Ukarabati wa barabara za ndani | • Kuchimba na kufukia mashimo na utoaji wa mifereji 1.5 km | 7,500,000/= | | |
| | | | • Kufyeka pande zote za barabara 2km | 4,500,000/= | | |
| 2 | MKUU | 1.Ujenzi wa barabara ya mkuu-bureni | • Kuchimba nusu km | 2,700,000/= | 1- | 1,500,000/= |
| 3 | MFINGA | 1.Ujenzi wa Barabara ya kwa Msheshi | • Kuchimba barabara | 8.000,000/= | - | |
| | | 2.Ukarabati wa | | 3,000,000/= | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | barabara ya kwa Mserego | • kukarabati | | | |
| 4 | **LAMBO** | 1.Ujenzi wa choo cha sekondari Ngolea | • Kumimina lenta na kumalizia ukuta wa choo . | 550,000/= | | 65,000/= |
| | | 2.Zahanati lambo | • Kumalizia upangaji wa mawe kwenye shimo la choo kwa mawe | 240,000/= | | |
| | | | • Kusakafia choo cha zahanati | | | |
| | | 3.Mradi wa maji | • Ununuzi wa kifaa cha maji mombea kilichoungua | 100,000/= | | 40,000/= |
| | | | | | - | |
| | | | | | | |
| 5 | **IBAYA** | 1.Ujenzi wa choo cha shule M/S Ibaya matundu nane | • Kipo hatua ya lenta mbao na tofali zimeshaandaliwa | 2,903,000/= | - | |
| | | 2.Ujenzi wa ofisi ya kijiji | • Msingi umejengwa nusu ,kokoto lori moja zimeshandaliwa | 2,440,000/= | | |
| 6 | **SHIGHATINI** | 1.Ujenzi wa madarasa 2S/M – | • Kupauwa na kupiga bati | 500,000/= | | 7,500,000/= |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Shighatini | | vyumba viwilivya madarasa | | | |
| | | 2.ukarabati wa choo cha wanafunzi s/m shighatini | | • Kurekebisha milango kutoa na kuweka mipya | 25,000/= | | |

**SEHEMU YA 6**

**CHANGAMOTO NA NAMNA YA KUKABILIANA NAZO KWA UJUMLA**

**1 .CHANGAMOTO**

(a) **UTAWALA;**

1. Jengo la ofisi ya kata limechakaaa sana na silingbodi linataka kuanguka kutokana na kuliwa na mchwa
2. Upungufu wa watendaji 4 ngazi ya Vijiji ktokana kukosa sifa na kuondolewa kwenye utumishi wa uma.

(b) **ELIMU**

**1. ukosefu wa maji shule ya sekondari kamwala**
2.Wananchi kutafsiri vibaya waraka wa utoaji wa elimu bure
3Watoto kutokula chakula mchana shuleni kwa baadhi ya shule
4.Ugumu wa michango ya walinzi wa shule za msingi na miundo mbinu na chakula kwa wanafunzi msingi na sekondari za kutwa
5.Upungufu wa walimu hasa katika shule ya msingi

(c) **AFYA**

1. kukosa Samani katika zahanati ya Mkuu
2. upungufu wa watumishi kwa baadhi ya vituo na nyumba za watumishi.
3. Upungufu wa vifaa tiba.

(d) **ULIZI NA USALAMA** .

1. Tunaendelea kutokomeza na kupambana na ulevi wa pombe hasa masaa ya kazi.

(e) **VIKAO VYA KISHERIA**

1. vikao vya vitongoji baadhi ya vitongoji bado havifanyiki

(f) **ARDHI NA MIPAKA**

1.Wajumbe wa mabaraza ya ardhi kutokuapishwa na kukosa semina elekezi
2.Kumuomba mkurungezi atume wataalamu ili kubaini mipaka hivyo
3.Kuomba semina elekezi kwa wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata zifanywe kwa kuleta ufanisi

(g) **KILIMO**

1. Ukosefu Wa Usafiri Kwa Afisa Ugani Kata Ili Kutembelea Eneo Lote La Kata Vijiji-6.
2. Vijiji Vinne Kukosa Maafisa Kilimo na mifugo – Mfinga, Shighatini,mkuu na Ibaya.

(h) **MAKUSANYO YA H/WILAYA**

1. Halmashauri ya wilaya kutokupeleka kwa wakati asimia 20% ya kijiji na 5% ya watendaji wa kata.

**2. MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

(a) **ELIMU;**

1.Kufanywa kwa vikao /mikutano:- ya wazazi kamati na bodi za shule, viongozi wa vijiji na walimu ili kuhamasisha uchangiaji wa chakula na michango mingine kama ya ujenzi wa miundo mbinu
2.Tunaomba fedha kutoka serikali kuu,H/wilaya,pamoja na michango ya wananchi ili kubiliana na tatizo hilo.

(b) **ULIZI NA USALAMA**

1. Kutoa elimu kwenye vikao/ na mikusanyiko mbalimbali na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaovunja sheria.
2. kusimamia sheria za uuzwaji wa pombe ili kumpunga hali hiyo

(c) **VIKAO VYA KISHERIA**

1. Kufanya vikao vya utendaji na kuhimiza watendaji kufanya vikao vyote vya kisheria na kusoma ripoti

(d) **KILIMO**

1. Kuendelea kuwashawishi na kuwaelimisha wananchi kutumia mbegu za kisasa na kilimo cha kisasa.

(e) **Makusanyo ya H/Wilaya**

1. kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili wafuatilie tin namba za biashara zao **T.R.A**

(d) **UTAWALA;**

1. Kuhimiza watendajiwa vijiji kupitia vikao vya utendaji kufanya kazi kwa ufanisi

**SEHEMU YA 8**

1. **MAPENDEZO.**

Tunaomba fedha kwa ajilii ya ukarabati wa jengo la ofisi ya kata kwani limechakaa sana na silingibodi linataka kuanguka na pia kuweka miundo mbinu ya umeme katika jengo hilo.

**HITIMISHO**

- Tunashukuru serikali kuu kutupatia fedha kwa ajiri ya ujenzi wa mabweni ,madarasa katika shule ya sekondari kamwala na tuko tayari kupokea wanafunzin wa kidato cha tano
- Tunaomba yale yote tuliyoyaomba kusaidiwa kutoka halmashauri ya wilaya yazingatiwe ili kuboresha ufanisi wa kazi katika eneo letu.

Naomba kuwasilisha.

……………………………………… ………………………………………

**ENEA H.MRUTU**
**DIWANI KATA YA SHINGATINI**

**GEOFREY J.NYANGERERERA**
**MTENDAJI KATA SHIGHATINI.**

AFISA MTENDAJI KATA SHIGHATI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA MAENDELEO KATIKA KATA YA KIVISINI ROBO YA KWANZA JULAY - SEPTEMBER -2017.

**UTANGULIZI.**

**MIPAKA**

Kata ya Kivisini Mashariki inapakana na Kata ya Jipe ,Magharibi ni Kata za Kileo na Mwanga, kusini inapakana na Kata za Kifula na Mwaniko

**UTAWALA.**

Kata ina Vijiji vitatu ambavyo ni Kivisini ,Kwanyange ,na Kitoghoto

**ELIMU.**

Kata ya Kivisini ina Shule tatu za Msingi ambazo ni Shule ya Msingi Kwanyange, Shule ya Msingi Kivisini na Shule ya Msingi Kitoghoto, zenye jumla ya wanafunzi 334.

**AFYA:** Kata ya kivisini ina zahanati moja ya kivisini inayotoa huduma.

**UCHUMI.**

Wakazi wa Kata ya Kivisini wanajishughulisha na kilimo, ufugaji, na biashara kidogo.

**ULINZI NA USALAMA.**

Hali ya Ulinzi na Usalama ni nzuri kwani wananchi wamekuwa wakijishughulisha na shughuli zao kwa amani na utulivu .Mahusiano kati ya wakulima na wafugaji ni nzuri.

**UVUVI HARAMU NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA.**

Kata ya Kivisini imekuwa katika jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira :

- Kukemea biashara haramu ya usafirishaji mkaa.
- Elimu inaendelea kutolewa juu ya uhifadhi wa mazingira na athari za uharibifu wa mazingira

**i)VIKAO NA MIKUTANO YA KISHERIA NGAZI YA KATA,VIJIJI NA VITONGOJI.**

| KATA | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIVISINI | 1 | 1 | - |

**ii)VIKAO VYA MIKUTANO YA KISHERIA YA VIJIJI.**

| | KIJIJI | VIKAO VYA H/VIJIJI | | MIKUTANO YA VITONGOJI | | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | LENGO | HALISI | LENGO | HALISI | |
| | KIVISINI | 3 | 3 | 6 | 2 | |
| | KWANYANGE | 3 | 3 | 6 | 4 | |
| | KITOGHOTO | 3 | 3 | 6 | - | |
| JUMLA | | 9 | 9 | 18 | 6 | |

**MAPATO NA MATUMIZI**

Kwa kipindi cha robo ya tatu taarifa ya mapato na matumizi zilizosomwa kwenye mikutano ni :

| KIJIJI | LENGO | HALISI | MENGINEYO |
|---|---|---|---|
| KIVISINI | 1 | 1 | |
| KWANYANGE | 1 | 1 | |
| KITOGHOTO | 1 | 1 | |
| **JUMLA** | **3** | **3** | |

**MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA**

Kwa kipindi hiki hukuna mapato yaliyokusanywa .

iii)**MAPATO YA HALMASHAURI ZA VIJIJI.**

Mapato ya halmashauri za vijiji yalikusanywa kama ifuatavyo:

| S/N | KIJIJI | LENGO | HALISI | ASILIMIA | MENGINEYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIVISINI | 1,500,000/= | 481,800/= | 32% | |
| 2 | KWANYANGE | 3,500,000/= | 3,105,000/= | 88% | |
| 3 | KITOGHOTO | 500,000/= | 287,000/= | 57% | |
| | **JUMLA** | **5,000,000/=** | **3,873,000/=** | **70%** | |

**MIRDI YA MAENDELEO NA TAARIFA ZA KISEKTA.**

**MIRADI YA MAENDELEO.**

| KIJIJI | JINA LA MRADI | HATUA MRADI ULIPOFIKIA | GHARAMA ZA MRADI | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | NGUVU ZA WANANCHI | H/WILAYA | S/KUU WAFADHILI | |
| KWANYANGE | Nyumba ya waalimu | Kupaua | - | - | 3,919,000/= | 3,919,000/= |
| KIVISINI | Ukarabati wa jengo la Zahanati ya Kivisini | | 1,241,500/= | - | - | 1,241,500/= |
| - | Ukarabati wa Kisima cha maji | Matengenezo ya Solary Solary | 6,000,000/= | - | - | 6,000,000/= |
| KITOGHOTO | Ujenzi wa zahanati | UKusanyaji wa michango | 287,000/= | - | - | 287,000/= |
| | | **JUMLA** | **7,528,500/=** | **-** | **3,919,000/=** | **11,447,500/=** |

iv)**TAARIFA ZA KISEKTA**

**SEKTA YA ELIMU.**

- Shughuli za ufundishaji zilifanyika kwa ufanisi kwa shule zote tatu .
- Kuhimiza wazazi kulipa fedha za chakula cha mchana kwa wanafunzi .
- Kufanyika kwa mtihani wa kuhitimu darasa la VII kwa Amani.

**SEKTA YA AFYA .**

(i) Elimu juu ya umuhimu wa kupima afya ili kujitambua iwapo umeambukizwa au la pamoja na mama wajawazito na wenza wao ilitolewa, waliopima ni ME 4 KE 13Jumla 17 .

ii) Mfuko wa afya ya jamii (iCHF)wanachama wapya waliojiunga ni (5).

**SEKTA YA KILIMO.**

- Shughuli za uvunaji mazao yaliyopatika zilifanyika .

**HALI YA CHAKULA.**

- Hali ya chakula siyo ya kuridhisha ni ya wastani.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII.**

- Shughuli za kuweka na kukopa katika vikundi mbalimbali zilifanyika .

**SEKTA YA MAJI.**

- Ukarabati wa kisima kirefu kinachotumia Solar Kijiji cha Kivisini ulifanyika..

**CHANGAMOTO.**

**Upungufu wa watumishi katika Kata .**

(i) Afisa afya .
(ii) Afisa Maendeleo Jamii.
(iii) Ukosefu wa walimu katika Shula za Msingi.

- Mwitikio mdogo wa wanaume kupima VVU na wenza wao
- Uchangiaji mdogo wa ICHF.
- Ushirikiano duni toka kwa wananchi juu ya uharibifu wa mazingira.
- Halmashauri kuchelewa kurudisha 100% mapato ya Kijiji.

**MIKAKATI.**

- Kuwahamasisha wananchi umuhimu wa kupima afya zao katika vijiji vyote
- Elimu ya upimaji VVU kuendelea kutolewa katika Zahanati.
- Kuwahamasisha wananchi kuchangia ICHF katika vijiji vyote.
- Kuendeleza mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira.
- Ukusanyaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Kufanya ukaguzi katika maeneo yenye uharibifu wa mazingira na kuwabaini waharibifu wa mazingira katika Vijiji.

**MAPENDEKEZO.**

- Halmashauri isaidie kuondoa kero ya upungufu wa watumishi katika Kata .
- Halmashauri isaidie mapambano ya uharibifu wa mazingira.
- Halmashauri irudishe mapato ya Vijiji kwa wakati.

**Nawasilisha**

[signature] ____________________ **MWENYEKITI**

[signature] ____________________ **KATIBU**